# Nipashe

Ijumaa Desemba 27, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580112

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Mwimbaji injili asakwa kwa tuhuma mauaji ya mkewe

UKURASA 2


Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

ARIGATOU INTERNATIONAL | GNRC | CEFA

2155447/02


RIPOTI MAALUMU

# Hivi ndivyo ilivyo rushwa ngono wasomi vyuo vikuu

UKURASA 4



Wakazi wa Jiji la Dar Salaam wakiwa Coco Beach kusherehekea Siku ya Zawadi (Boxing Day) jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## Askofu ataka tume huru uchaguzi

UKURASA 22

## 40,000 kuajiriwa serikalini Februari

• **Mishahara** watumishi 6,000 kupanda mwezi ujao... *Endelea ukurasa 2*




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


**MICHEZO** SIMBA SC YAPANGA HESABU LIGI KUU UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Aliyepokea rushwa 50,000/- ahukumiwa kulipa mil. 1/-

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

OFISA Utumishi wa Kampuni ya Sino Hydro Power, Baraka Elias, amehukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni moja baada ya kukutwa na hatia ya kuomba rushwa ya Sh. 50,000 kutoka kwa mwendesha mitambo wa kampuni hiyo.

Mahakama ya Wilaya ya Kibiti, ilimhukumu Baraka kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. milioni moja, baada ya kukutwa na kosa la kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 50,000, kinyume na kifungu 15(1)(a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya Mwaka 2007.

Awali, mwendesha mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Beatrice Ngago, akisoma mashtaka mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Kibiti, Florian Mtulo alisema, mshtakiwa alitenda kosa la kushawishi kuomba rushwa ya Sh. 50,000.

Imedaiwa kuwa, mtuhumiwa huyo ambaye ni Ofisa Utumishi wa kampuni hiyo inayojenga mradi wa kitaifa wa umeme, katika Mto Rufiji, aliomba rushwa kwa Wilfred Rutibi, ambaye ni mwendesha mitambo ili asimfukuze kazi. Kwa mujibu wa mwendesha mashtaka, mtuhumiwa alimweleza mlalamikaji kuwa hakupaswa kuajiriwa katika kampuni hiyo, kwa kuwa alishawahi kuajiriwa katika Kampuni ya CRDC, ambayo pia inajenga mradi wa umeme Rufiji na kufukuzwa kazi, hivyo alipoteza sifa za kuajiriwa.

Ilidaiwa kuwa, mtuhumiwa alikamatwa Desemba 22, na maofisa wa Takukuru kituo maalumu cha Ikwiriri kwa kushirikiana na askari wa Jeshi la Polisi, baada ya kuandaliwa mtego na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa akiwa kazini eneo la mradi.

Baraka alikiri makosa yote mawili, kuomba na kupokea rushwa, na baada ya kulipa faini aliachiwa huru.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, ametoa wito kwa wakazi wa mkoa huo kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kuondoa kero hiyo ambayo imekuwa ikichangia baadhi ya huduma kutofanyika kwa ufanisi.



Wananchi wa Mtaa wa Pambogo katika Kata ya Iyela jijini Mbeya, wakionyesha mipaka ya eneo lao na uwanja wa ndege wa zamani wa Mbeya, ambalo wanadai wanataka kuporwa na Halmashauri ya Jiji. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# 40,000 kuajiriwa serikalini Februari

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Laurean Ndumbaro, amesema serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya zaidi ya 40,000 katika kada mbalimbali Februari mwakani.

Dk. Ndumbaro aliyasema hayo jijini hapa alipojibu maswali ya waandishi wa habari waliohoji mikakati ya serikali kukabiliana na tatizo la uhaba wa watumishi katika kada ya afya.

Alisema serikali katika mwaka wa fedha 2019/20, imepanga kuajiri watumishi wapya zaidi ya 40,000 katika kada mbalimbali.

"Katika mwaka wa fedha 2019/20, serikali imetenga idadi hiyo ya ajira ambazo zitaanza kutolewa Februari 2020, zikiwamo za kada ya afya ambazo zitasaidia kukabiliana na uhaba wa watumishi katika baadhi ya vituo vya afya na hospitali nyingi zilizojengwa katika awamu hii ya tano," alisema.

Katibu Mkuu pia alizungumzia upandishwaji wa vyeo kwa watumishi wa umma waliokidhi vigezo, akieleza kuwa ofisi yake ilitoa idhini kwa waajiri kutekeleza suala hilo kwa mwaka 2017/18 na ubadilishwaji wa vyeo kwa mwaka wa fedha 2018/19.

"Katika utekelezaji wa zoezi hili, hadi sasa watumishi 95,905 waliokuwa na sifa kwa mujibu wa sheria na kanuni za utumishi pamoja na miundo ya utumishi, wamebadilishwa mishahara yao katika mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara (HCMIS) na taarifa za watumishi 6,000 zilizobakia zinaendelea kufanyiwa kazi na zitakamilika Januari 2020," alisema.

Alisema upandishwaji wa vyeo kwa watumishi wanaostahili na walio katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 na 2019/2020 utafanyika ndani ya mwaka huu wa fedha baada ya kukamilisha uidhinishwaji tajwa.

Alisema Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pia imebaini kuna waajiri wanaowasilisha katika ofisi yake taarifa za uongo kuhusu upandishwaji vyeo kwa watumishi kwa nia ovu.

Alisema taarifa hizo zinatumwa na waajiri zikitaka watumishi wao wapandishwe vyeo bila kutimiza vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazosimamia utumishi wa umma.

Aliwaonya viongozi pamoja na wakuu wa taasisi za umma ambao wamekuwa wakijihusisha na tabia hizo, akiwataka kuacha mara moja kwa kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi yao ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi.

# Mwimbaji nyimbo za injili asakwa madai kuua mkewe

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

VYOMBO vya ulinzi na usalama katika Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, vinaendesha msako mkali wa kumtafuta Mosses Pallangyo, mwimbaji wa nyimbo za injili anayetuhumiwa kumuua mkewe Marry Mushi kwa shoka.

Akizungumza jana katika Kijiji cha Kilinga wilayani humo, baada ya kutembelea kuona mauaji hayo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Jerry Muro, alisema alifika muda mchache eneo la tukio baada ya tukio hilo kutokea.

"Kweli nimesikitishwa sana na tukio hili lililotokea siku ya Sikukuu ya Krismasi nawapa pole wananchi wa kijiji hiki kwa tukio hili baya lililoharibu sikukuu yetu," alisema.

Kwa mujibu wa Muro, tayari vyombo vya dola vimeanza msako mkali kumtafuta mtuhumiwa ili atiwe mbaroni.


"Nawaomba wananchi muwe watulivu na mtuachie vyombo vya usalama tulifanyie kazi na wananchi wanaofahamu mahali alipokimbilia mtuhumiwa wasaidie vyombo vya dola kuvipa taarifa," alisema.

Baba mzazi wa mtuhumiwa, Latiaeli Pallangyo, alisema tukio hilo lilitokea Desemba 25, mwaka huu majira ya mchana.

Alisema Marry (marehemu) na mwanawe Mosses wana wiki tatu tangu waanze kuishi pamoja kama mume na mke.

"Lakini hapakuwa na ugomvi wowote na tulitegemea watasherehekea Sikukuu ya Krismasi vizuri na asubuhi kabla ya kutokea mauaji haya Marry alipika chai na kuendelea na shughuli za kawaida mpaka mauti yalipomfika kwa kupigwa na shoka chumbani kwake," alisema.

## HABARI KITAIFA



Ofisa Takwimu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Makunga Seleman (kulia), akishuhudia mifugo ya wananchi wa Kata ya Igurusi wilayani Mbarali ikiogeshwa wakati wa ziara yake ya kuhamasisha uogeshaji wa mifugo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Uwekezaji kadi za kielektroniki sasa watajwa kukuza uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZA) imesema inaendelea kuvutia uwekezaji kwenye viwanda vinavyotumia teknolojia ya kisasa ili kukuza na kuendeleza wajasiriamali waweze kuitumia na kukuza uchumi.

Mkurugenzi wa Uhamasishaji Uwekezaji wa EPZA, James Maziku, alisema hayo alipokuwa anazungumzia uwekezaji wa kiwanda cha kutengeneza kadi za kielekTroniki cha 'DZ Cards' Afrika kilichopo katika eneo maalum la uwekezaji la Benjamin William Mkapa, jijini Dar es Salaam. Uwekezaji katika kiwanda hicho pekee kilichopo Afrika chini ya Jangwa la Sahara ni zaidi ya Sh. bilioni 11.

Baadhi ya viwanda vilivyopo katika maeneo maalum ya uwekezaji EPZ ni pamoja na viwanda vya nguo, vinavyochakata nafaka, vya kutengenezea vifungashio, vifaa vya ujenzi na vya bidhaa za ngozi. Maziku alisema kuongezeka kwa mahitaji ya kadi za kielektroniki na kukuza uchumi usiotumia pesa taslimu ndio imefanya kiwanda cha DZ Cards Afrika kupanua masoko ili kusambaza bidhaa zake katika bara lote la Afrika.

"Ongezeko la mahitaji ya kadi za kielektroniki na kukuza matumizi uchumi usiotumia pesa taslimu ndio imetoa

INAENDELEA UK. 8

# Abiria wakoshwa treni Dar-Moshi

**Na Maulid Mmbaga**

ABIRIA wanaosafiri kwa treni ya Dar es Salaam-Moshi, wameeleza kufurahishwa na huduma hiyo iliyorejeshwa mwanzoni mwa mwezi huu, baada ya kusimama kwa miaka 25.

Treni hiyo ilianza tena safari zake Desemba 6, mwaka huu, safari moja kwa sasa ikichukua zaidi ya abiria 600 na imepunguza adha kwa wananchi hasa wazaliwa wa Mkoa wa Kilimanjaro ambalo wana utamaduni wa kurejea walikozaliwa kwa ajili ya mapumziko ya mwishoni mwa mwaka.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alisema jana kuwa serikali inajitahidi kuhakikisha inaboresha huduma ya usafiri huo hususani kipindi hiki cha sikukuu. Alisema katika mikakati yake, serikali imeagiza mabehewa 44 ili kukidhi mahitaji ya kuwa kumekuwa na idadi kubwa ya abiria kwa kipindi hiki cha mwisho wa mwaka.

"Ruti ya kutoka Dar es Salaam kwenda Moshi ni Jumanne na Ijumaa, Moshi kwenda Dar ni Jumatano na Jumamosi, safari inaanza saa 10:00 alasiri na kufika 2:00 asubuhi," alisema.

"Ruti ya Moshi tulitakiwa tupeleke treni kila siku. Jana (juzi) tulibeba abiria 950, kutoka Dar es Salaam kwenda Moshi, hivyo ni dhahiri kwamba uhitaji wa huduma hii ni mkubwa," alibainisha.

Alisema huduma ya usafiri wa treni itaendelea kutolewa pia katika mikoa ya Mwanza, Tabora na Kigoma ikiwa ni jitihada za serikali katika kurahisisha usafiri kwa wananchi.

Mmoja wa abiria wa treni ya Dar es Salaam kwenda Moshi, Eveline Lyimo, alipongeza serikali kwa kurejesha usafiri huo kwa Mkoa wa Kilimanjaro baada ya

INAENDELEA UK. 8

# Kifo mjamzito, mwanawe mtoni chaibua kinamama

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

BAADA ya mjamzito Maria Kalunde (42) na mwanawe Magreth Lui (9), kufa maji wakati wakivuka Mto Kalambo akimsindikiza mama yake kwenda kliniki, baadhi ya wanawake wa Kijiji cha Kasitu wilayani Kalambo mkoani Rukwa, wameiomba serikali kujenga daraja katika mto huo ili waache kuhatarisha maisha yao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na gazeti hili wanawake hao walisema wamekuwa wanakabiriwa na changamoto kubwa hasa kipindi cha masika kuvuka mto huo, kwa kuwa hujaa ma wakati mwingine maji hupita juu ya kivuko cha miguu kinachokatisha mto huo.

Mmoja wa wanawake hao, Isabella Sinyangwe, alisema katika msimu wa mvua nyingi, wanawake wamekuwa wakikabiliwa na wakati mgumu kwa kuwa huduma nyingi zikiwamo za afya zinapatikana ng'ambo baada ya kuvuka mto huo.

Alisema kuna baadhi ya siku wamekuwa wazilazimika kukosa huduma hizo kutokana na maji kujaa hadi kupita juu ya daraja,

INAENDELEA UK. 8



**RIPOTI MAALUM**

# Hivi ndivyo ilivyo rushwa ngono wasomi vyuo vikuu

## •Mshika sheria, mtenda, mtendwa waanika...

**Na Sanula Athanas**

HIVI sasa kuna kilio cha wigo mpana wa rushwa kuingia katika mustakabali wa elimu, hususan ngazi ya vyuo vikuu kunakoripotiwa matukio yenye ushahidi.

Picha ya wazi ya kashfa hiyo iko zaidi kati ya mwalimu na mwanafunzi wake, lakini kwa upande wa pili wa sarafu, inafanyika kati ya wanafunzi wenyewe.

Ni madhara yanayogusa kila kona, kuanzia mamlaka rasmi za kiserikali na zisizo za kiserikali, kwa maana ya jamii kwa tafsiri yake pana, ujumbe mkuu ni kwamba 'elimu ndiyo kioo cha jamii' na mahali panapotumika kuunda msingi wa jamii ya sasa na taifa liendako.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), inaegemeza tafsiri yake rasmi kuhusu rushwa kwa kurejea Kamusi ya Kiswahili Sanifu, toleo la mwaka 2004, ikifafanua: "Ni fedha au kitu cha thamani kinachotolewa na kupewa mtu mwenye madaraka ya jambo fulani ili mtoaji apatiwe upendeleo."

Inaendelea na ufafanuzi wake kwamba: "Rushwa ni matumizi mabaya ya ofisi au mamlaka kwa manufaa binafsi, na mara nyingi hutolewa kwa siri kwa sababu ni tendo la fedheha na ni kosa la jinai.

"Matokeo ya vitendo hivi vya rushwa ni kuathirika kwa upatikanaji wa huduma za kijamii ambazo ni haki ya wananchi ambapo huduma huwa duni au kutopatikana kabisa."

Vivyo hivyo, wanataaluma katika nafasi yao, wanaitafsiri dhana ya elimu kuwa ni tendo au uzoefu wenye athari ya kujenga akili, tabia au uwezo wa kimaumbile wa mtu binafsi.

Wasomi hao katika tafsiri ya kiufundi, wanaeleza kwamba elimu inabeba maana ya njia inayotumiwa kwa makusudi na jamii kupitisha maarifa, ujuzi na maadili kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Ili kufanikisha urithi huo, wataalamu wanaobeba jukumu la kuratibu na kusimamia mchakato wa elimu wanaitwa walimu. Hao wanawajibika chini ya chombo maalum cha kitaaluma kufanikisha lengo linalopitishwa katika mitaala na muhtasari wa masomo (syllabus).

Kwa kurejea maeneo yao mahsusi ya kiutendaji, walimu hao wamebatizwa majina mbalimbali ya vyeo na wajibu, kulingana na kiwango wanachowajibika. Hilo ndilo linalozaa majina kama profesa, mhadhiri na mkufunzi.

Hali kadhalika, dhana ya ngono inayolalamikiwa kuchukua nafasi ndani ya elimu, inatafsiriwa katika Kamusi ya Oxford kwamba ni: "Tendo la mwanamke na mwanamume kujamiiana."



**TAKUKURU vs KINACHOJIRI**

Inaelezwa kuna mtazamo mpana zaidi unaotawala nyendo na vyanzo vya rushwa ya ngono vyuoni, ambavyo ushahidi na mazingira yake ni mambo dhahiri.

Matukio yanayojitokeza, tabia zilizotawala na aina ya utamaduni ulioshika kasi, ni miongoni mwa viwasilisho vya ushahidi huo.

Mathalani, inapotokea mamlaka ya chuo cha elimu ya juu kukiri matukio hayo, baadhi ya wahadhiri wake kukumbwa na kesi za kashfa hiyo, wanafunzi ama kulalamika au kuanika kwa njia rasmi na zisizo rasmi, huku wenye dhamana ya kuwasimamia nao wakiweka wazi namna wanavyoona shida ya ukakasi huo, ni kielelezo kingine.

Kwa kurejea Oktoba mwaka jana, Takukuru ilitangaza kumshikilia mhadhiri (jina tunalihifadhi) wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), aliyetuhumiwa kuomba rushwa ya ngono kutoka kwa mwanafunzi wake.

Ni tukio lililofungua rasmi picha mbaya kwa chuo hicho kinachotikisa kwenye orodha ya ukubwa barani Afrika, pia kikishika rekodi ya juu ya uwekezaji kielimu katika awamu iliyopita ya uongozi wa serikali.

Wakati Takukuru ikiwa katika tafakuri ya mageuzi hayo yanayohusu aina hiyo mpya ya rushwa kwa wasomi wa daraja la juu, kuna lingine limeibuka jijini Dar es Salaam na kupatiwa ushahidi uliotumika kulifikisha mahakamani.

Leo inatimu mwezi mmoja, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam ilipomhukumu mhadhiri wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), mwenye umri wa miaka 69 (jina tunalo), kutumikia jela miaka mitatu.

Katika kesi hiyo ambayo hukumu yake ilisomwa Novemba 27, mwaka huu, kosa kuu lililomtia hatiani ni kunaswa na Takukuru alipoomba rushwa ya ngono kutoka kwa wanafunzi wake.

Mhadhiri huyo wa chuo hicho pekee mahsusi kwa sekta ya usafirishaji nchini, ambaye mkasa wake ulisababisha kutapakaa mjadala wa kijamii kitaifa, alinusurika kifungo, baada ya kutumia fursa ya makubaliano na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), alipokiri kutenda kosa, kuomba msamaha na kulipa faini ya Sh. milioni tano.

Katika mkasa mwingine unaofanana, Machi 5 mwaka huu, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, alilazimika kuzuru Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (SAUT) jijini Mwanza, kushughulikia malalamiko ya baadhi ya wanafunzi waliodai kunyanyaswa kingono na wahadhiri.

Ole Nasha alifanya kikao cha ndani na uongozi wa chuo, kisha akakutana na baadhi ya wanafunzi na uongozi wa serikali ya wanafunzi kwa faragha, viongozi wa SAUT wakiwa nje ya ukumbi ili kuwapa wanafunzi uhuru wa kujieleza.

Kupitia mkutano huo, Naibu Waziri alibaini matatizo makuu matano yanayowakabili wanafunzi, kubwa likiwa ukatili wa kijinsia dhidi yao, mzizi mkuu akitaja wahadhiri kukosa uaminifu na kuendekeza rushwa kutoka kwa wanafunzi.

"Wakati wanachuo wakijieleza, nilibaini mambo makuu matano yanayowakabili ambayo ni ukosefu wa mifumo sahihi ambayo inatumiwa chuoni, kuwapo baadhi ya walimu wanaoomba rushwa kwa wanafunzi ili kuwaongeza ufaulu," Ole Nasha alisema.



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (SAUT). Prof. Costa Mahalu.

Kiongozi huyo wa elimu nchini anafafanua kwamba, ukosefu wa bima ya afya kwa wanafunzi waliokwishalipa, ubadhirifu katika ofisi ya mikopo chuoni na uongozi kutotoa ushirikiano kwa wanafunzi wenye matatizo, ni sehemu ya mzizi wa madhila.

Kwenye majumuisho yake, Ole Nasha alimwagiza Katibu Mkuu wa wizara yake, kufanya uchunguzi maalum utakaosaidia kuibua ukweli uliojificha kuhusu dodosa za kashfa hiyo na hatua za kuishughulikia.

Katika mwitikio wake, Makamu Mkuu wa SAUT, Profesa Costa Mahalu, anasema wameanzisha kitengo maalum cha kupokea malalamiko ya kijinsia katika taaluma, ikijumuisha suala la rushwa ya ngono, kwa kuwa tuhuma hizo zinakinzana kwa asilimia 100 na malengo ya kielimu na kiroho ya kuanzishwa kwa taasisi hiyo.

Profesa Mahalu, ambaye kitaaluma ni mwanasheria, anasema taratibu za kupokea malalamiko zinajumuisha kwa mdomo na kimaandishi, huku akikiri uwezekano wa kuwapo suala hilo ambalo SAUT katika msimamo wake rasmi inalitafsiri kuwa tendo ovu.

Anaendelea: "Napata ugumu kusema lipo hapa au halipo. Lakini, malalamiko yapo, ila ushahidi unakuwa mgumu sana. Uhusiano ni wa watu wawili, lakini mmojawapo anaposhindwa kuelewana na mwenzake, huibuka hadharani.

"Hapa SAUT tuna kitengo cha 'social ethics' (maadili ya jamii), wanafunzi wa mwaka wa kwanza wanapofika tu, tunawapa elimu ya namna ya kuishi chuoni na maadili yake, maana wapo baadhi ya wanavyuo wanapopata uhuru wa kujiamulia, hasa wale ambao hawajalelewa katika maadili mema, hufanya mambo ya ovyo.

"Pia, tumewaelekeza watawa wetu na mapadri wetu kuwajaza elimu ya maadili. Hayo ni matukio machache tu ambayo yanachafua vyuo, lakini hapa SAUT kama mnavyoshuhudia, tuna wanafunzi zaidi ya 13,000. Idadi hii ni kubwa na inatokana na ubora wa elimu tunayoitoa hapa.

"Nia yetu ni kuona malengo tuliyojiwekea yanatimia, ikiwa ni kuwa chuo cha mfano Afrika, ambacho kinatoa wabobezi wa kada mbalimbali, wanaohimili ushindani katika soko la ajira duniani," anatamba.

ITAENDELEA KESHO

# MATANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA

### TAREHE YA MWISHO YA MSAMAHA MAALUM WA KODI KWA MUJIBU WA AGIZO NAMBA, 282A, 2018 YA MSAMAHA WA RIBA NA ADHABU

**Dar es Salaam, 19 Desemba 2019:**
Mamlaka ya Mapato Tanzania (Ijulikanayo kama"TRA" au "Mamlaka") inapenda kuwakumbusha walipakodi wote kwamba mnamo tarehe 14 Juni 2018, Waziri wa Fedha na Mipango alitangaza msamaha maalum wa riba na adhabu chini ya **AGIZO Namba 282A, 2018 ya msamaha wa Riba na Adhabu** kwa walipakodi wenye malimbikizo ya madeni ya kodi na wale ambao kwa hiyari yao waliweka wazi au kuthibitisha malimbikizo ya madeni yao ya Kodi na walikuwa tayari kulipa malimbikizo hayo ya kodi ya msingi katika kipindi na masharti yaliyowekwa na AGIZO hilo.

Msamaha huo wa kodi ulibuniwa ili utekelezwe ndani ya muda maalum ukianzia **tarehe 1 Julai 2018 hadi 30 Juni 2019**. Hata hivyo, kulingana na sababu za msingi, Serikali kupitia **Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu),** (Nyongeza ya muda wa Kulipa), 2019, iliongezea muda wa malipo ya Kodi ya msingi kufikia tarehe 31 Desemba 2019, kwa walipakodi ambao: -

a) Waliomba msamaha wa riba na adhabu za kodi kwa Kamishna Mkuu;
b) Walipatiwa msamaha wa riba na adhabu;
c) Walioingia makubaliano na Kamishna Mkuu ya kusamehewa riba na adhabu za kodi kama ilivyo ainishwa katika **AGIZO Namba 282A, 2018 ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi (msamaha wa Riba na Adhabu).**
d) Walikubali kulipa Kodi ya msingi iliyokadiriwa kwa mkupuo au kwa awamu; na
e) Wale ambao mpaka tarehe **30 Juni 2019,** alishindwa kulipa kwa ukamilifu, kiasi cha kodi ya msingi kilichokubaliwa.

Hivyo, walipakodi wote waliopewa msamaha wa riba na adhabu wanakumbushwa kutumia fursa hii kumalizia madeni yao ya kodi ya msingi kabla ya au **tarehe 31 Desemba 2019** kama ilivyoainishwa katika makubaliano. Izingatiwe kwamba, mlipakodi yoyote ambaye atakuwa amepewa msamaha chini ya **AGIZO namba 282A, 2018 ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu),** na akashindwa kukidhi au kutekeleza masharti ya mkataba wa makubaliano ya malipo, Kamishna Mkuu atabatilisha mkataba wa makubaliano na kudai kiasi cha kodi ya msingi kilicho salia pamoja na riba, na adhabu kama vile hakukuwa na masamaha uliotolewa.

Aidha kwa taarifa hii ya mwisho, walipakodi wote wanajulishwe kwamba, kuanzia **tarehe 1 Januari 2020,** Kamishna Mkuu atachukua hatua za kukusanya kodi dhidi ya walipakodi wote walioshindwa kuheshimu msamaha uliotolewa na kukusanya kodi stahiki, riba, na adhabu zote BILA taarifa nyingine zaidi ya hii.

**Kwa taarifa hii, tekeleza kama ilivyoelekezwa.**

**"Pamoja Tunajenga Taifa letu"**

**Msafiri Mbibo.**
**KAIMU KAMISHNA MKUU**

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA

### MAWASILIANO YA KIKODI BAINA YA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA NA WAWAKILISHI WA WALIPAKODI

**Dar es Salaam, Desemba 20, 2019**

Mamlaka ya Mapato Tanzania ("TRA" au "Mamlaka") inatambua na kuthamini umuhimu wa mawasiliano, kwa njia ya majadiliano, yanayohusu masuala ya kikodi baina ya Mamlaka yenyewe na walipakodi wetu. Kimsingi, majadiliano haya ni moja ya nguzo za kutusaidia TRA katika kutekeleza kwa ufanisi jukumu letu la kukadiria, kukusanya, na kuhasibu kodi ya Serikali. Pia, kupitia majadiliano haya, walipakodi hupata fursa ya kupata uelewa mkubwa ili kuwasaidia kutekeleza wajibu wao wa kisheria wa kulipa kodi kwa hiari na kwa wakati.

Vile vile, tunapenda kuwataarifu walipakodi na wananchi kwa ujumla kuwa, kwa mujibu wa **Kifungu cha 27(1)(a) cha Sheria Na. 10 ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015,** mlipakodi ana haki ya kuwakilishwa na mwakilishi atakayemteua kwa ajili ya majadiliano baina ya TRA na mlipakodi husika. Hata hivyo, kwa kuwa taarifa za mlipakodi ni siri baina ya mlipakodi na TRA (kama ilivyoelekezwa katika **Kifungu cha 21 cha Sheria tajwa),** uwakilishi wowote tofauti na mlipakodi mwenyewe ni sharti uzingatie matakwa ya **Kifungu cha 27(1)(b) cha Sheria** tajwa ambapo ni lazima mlipakodi amtaarifu, kwa maandishi, Kamishna Mkuu wa TRA kuhusu uwakilishi huo. Ikumbukwe kwamba, mtu yeyote ambaye ama si Mmiliki au Mkurugenzi wa kampuni (mlipakodi), hana uhalali wa kumwakilisha mlipakodi iwapo hana Hati ya Uwakilishi (Power of Attorney), kutoka kwa mlipakodi, ambayo itawasilishwa TRA baada ya kufuata taratibu zote za kisheria, ikiwa ni pamoja na kusajiliwa na Msajili wa Hati (Registrar of Documents).

Aidha, wawakilishi Wataalam, kama vile Mawakili (Advocates), wanaweza kuwawakilisha walipakodi kama wateja wao endapo wateuliwa rasmi na wateja hao na uteuzi wao kutaarifiwa kwa Kamishna Mkuu kwa mujibu wa Kifungu cha 27(1)(b) cha Sheria tajwa kama ilivyofafanuliwa hapo juu. Kwa upande wa wawakilishi ambao ni Wataalam Elekezi wa Kodi **(Tax Consultants),** kama Kifungu cha 28 cha Sheria tajwa kinavyotambua uwepo wao, ni lazima wawe wamesajiliwa na Mamlaka kwa mujibu wa Kanuni ya 5 ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi za mwaka 2016.

Kwa upande wa masuala ya forodha yanayosimamiwa na TRA kupitia Idara yake ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa, **Kifungu cha 6 cha Sheria Na. 10 ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015** kinampa Kamishna Mkuu mamlaka ya kutumia vifungu vya Sheria hiyo kwenye masuala ya forodha endapo matumizi ya Sheria hiyo hayakinzani na utaratibu uliowekwa na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Hivyo, Mawakala wa Forodha (waliosajiliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 145 na kwa kuzingatia matakwa ya **Kifungu Na. 146, 147 na 148 cha Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004),** Mawakili, na Wawakilishi wowote watatambuliwa rasmi kama wawakilishi wa walipakodi iwapo taarifa za uteuzi wao zitawasilishwa kwa Kamishna wa Forodha. Aidha, tunaomba ieleweke kwamba kitambulisho cha mfanyakazi (Identity Card) au sare ya kazi sio kibali cha uwakilishi halali kwa mujibu wa Sheria.

Hivyo, natoa wito kwa walipakodi na wananchi kuzingatia ufafanuzi huu kwa lengo la kuwa na majadiliano baina ya TRA na walipakodi yanayotambulika kisheria. Tunaomba ieleweke kwamba ushiriki wa watu ambao si wawakilishi halali wa walipakodi, sio tu ni uvunjifu wa matakwa ya **Kifungu cha 21 cha Sheria Na. 10 ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015,** kwa upande mmoja, lakini pia, kwa upande mwingine, husababisha majadiliano mengi yasiyo na tija na ambayo ama huwa hayafikii muafaka au hufikia muafaka usiokubalika kisheria na walipakodi husika wanapopelekewa maamuzi ya kikodi.

**Tunatanguliza shukrani kwa ushirikiano.**

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Msafiri Mbibo.**
**KAIMU KAMISHNA MKUU**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni wakati mwafaka kuachana kabisa na uagizaji mbegu nje

**UPATIKANAJI** wa mbegu bora za kilimo umekuwa moja ya changamoto ambazo zinawakwaza wakulima wetu.

Wakulima wengi wakati mwingine wanashindwa mahali za uhakika pa kuzipata, lakini gharama yake ni kubwa, hivyo kuwa miongoni mwa sababu za kushindwa kuzipata.

Hata hivyo pamoja na changamoto ya upatikanaji wa mbegu za kisasa kwa wakulima wetu nchini, katika miaka ya karibuni zimekuwapo jitihada mbalimbali ambazo zinaendelea za uzalishaji wa mbegu za kisasa zinazofanywa na taasisi zetu za utafiti wa kilimo.

Taasisi hizi zinaendelea kuzalisha mbegu bora na za kisasa za mazao mbalimbali ya chakula na biashara, hivyo kuashirika kwamba nchi yetu kwa sasa haina sababu za kuagiza mbegu kutoka nje.

Pengine ni kutokana na jitihada hizi, serikali imeona kuwa kwa sasa hakuna sababu za kuendelea kuagiza mbegu kutoka nje kwa kutumia fedha nyingi.

Kutokana na hali hiyo, serikali ilieleza mwishoni mwa wiki iliyopita kuwa imekusudia kuanzisha juhudi wezeshi kuwezesha mbegu bora za kilimo kuzalishwa nchini ili kuondokana na wimbi la uagizaji wa mbegu nje ya nchi.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, baada ya kutembelea kampuni ya Namburi inayojihusisha na uzalishaji wa mbegu za mahindi, mtama na mpunga iliyopo katika eneo la Vwawa wilayani Mbozi wakati akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Songwe.

Alisema kuwa Tanzania ina uhitaji wa mbegu kiasi cha tani 186,000 za mazao mbalimbali, huku uzalishaji wa ndani ikiwa ni pamoja na uagizaji wa mbegu nje ya nchi ukiwa bado mdogo kwani haujafikia hata tani 50,000.

Alibainisha kuwa Tanzania ina maeneo makubwa na bora kwa uzalishaji, hivyo ni lazima kuzalisha mbegu za kutosha nchini na kuachana na utegemezi wa mbegu kutoka nje ya nchi.

Waziri Hasunga aliwataka wananchi kuhakikisha kuwa wananunua mbegu bora kwa ajili ya kukabiliana na msimu wa kilimo na kuachana na matumizi ya mazao yao ya msimu iliyopita waliyoyahifadhi kama mbegu.

Kutokana na jitihada na kasi kubwa ya utafiti na uzalishaji wa mbegu bora nchini, tunaona kwamba uamuzi wa serikali wa kuagiza mbegu kutoka nje ni hatua nzuri ya kuboresha kilimo chetu nchini.

Kilimo hiki ndicho tegemeo la kusapoti viwanda ambavyo vimeanza kujengwa kwa lengo la kuipeleka Tanzania katika uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

Kwa hiyo kama taifa ni hatua nzuri ya kuachana na utaratibu wa kuagiza mbegu kutoka nje ambao hauna tija kwa sababu miongoni mwa kasoro zake ni kuagiza kiasi ambacho hakilingani na mahitaji halisi.


Kibaya zaidi ni kuwa uhaba wa mbegu bora na za kisasa unawafanya wakulima kutegemea mbegu walizozizalisha misimu ya nyuma, ambazo mara nyingi hazina ubora na matokeo yake ni kuchangia kushuka kwa mavuno kila mwaka.

Tunaamini kuwa serikali haitarudi nyuma katika uamuzi wake wa kujielekeza katika uzalishaji wa mbegu baada ya kuziagiza nje.

Ushauri wetu ni kuwa serikali katika kutekeleza mpango huu ishirikishwe taasisi za utafiti wa kilimo ambazo zimefanya utafiti wa kina wa mbegu pamoja na kuzizalisha. Kwa kufanya hivyo tutazalisha mbegu bora na za kukidhi mahitaji ya wakulima nchini.

Aidha, utekelezaji wa mpango huu uwashirikishe maofisa ugani wetu kwa kiwango kikubwa, ikiwamo kuwapeleke kwa wakulima kwa ajili ya kuwapa elimu kuhusu matumizi ya mbegu hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kampeni hizi zinaweza 'kufuta' jembe la mkono

Na Sabato Kasika

**KILIMO** cha kutumia jembe la mkono na kinachotegemea mvua za msimu ndicho kinachotumiwa na wakulima nchini na kwa namna moja au nyingine, kinachangia kukwamisha maendeleo yao.

Kutokana na hali hiyo, wadau wa kilimo kwa kushirikiana na serikali wamekuwa wakiendesha mikakati ya kuwezesha kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya kuimarisha kilimo cha umwagiliaji.

Serikali nayo iko katika mkakati wa kuondoa jembe la mkono, ili wakulima watumie matrekta yanayoweza kuwafanya wakidhi mahitaji kwenye kilimo.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC), Profesa Damian Gabagambi, alikaririwa na vyombo vya habari kwamba NDC, inataka jembe la mkono libaki katika Makumbusho ya Taifa.

Hatua hizo za NDC ni nzuri, kwani zina mwelekeo wa kusaidia kumkomboa mkulima kutoka katika matatizo anayokabiliana nayo kwa jembe la mkono na kutegemea mvua za msimu. Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, inasema zaidi ya asilimia 66 ya Watanzania ni wakulima wengi wa wanatumia jembe la mkono na kutegemea mvua za msimu kwa ajili ya kilimo.

Kilimo cha kutegemea jembe la mkono hakiwezi kukidhi mahitaji ya chakula au kwenye mazao ya biashara, hivyo ni muhimu wakulima waachane na jembe hilo ambalo limekuwapo tangu nchi ipate uhuru.

Suala la uimarishaji wa kilimo linasisitizwa sana na serikali, kwani hata Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amewahi kusema, ni moja kati ya juhudi za serikali za kuboresha shughuli za kiuchumi katika taifa.

Asilimia 75 ya wananchi wanajihusisha na kilimo, mifugo na uvuvi nchini na kusisitiza, serikali itaendelea kuzipa kipaumbele sekta hizo na kuongeza bajeti, ili ziongeze pato la taifa na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Serikali imeweka mikakati inayolenga kusaidia uimarishaji wa shughuli za kilimo kwa kuongeza matrekta makubwa na madogo kutoka 7,491 mwaka 2005/2006 hadi 16,478 kwa mwaka wa fedha 2016/2017, hivyo kupunguza matumizi ya jembe la mkono kutoka asilimia 70 hadi asilimia 12.

Nikirejea kwenye lengo langu ni kwamba, wakati serikali ikiwa na mpango wa kuongeza matrekta, mmoja wa wadau wa kilimo Prof. Sospeter Muhongo amekuja na mkakati wa kuwatua wakulima jembe la mkono jimboni mwake.

Mkakati huo ni kugawa majembe 20 ya kukokotwa na ng'ombe (plau), kwenye vijiji vya Jimbo la Musoma Vijijini, lengo ni kuhakikisha wakulima wanaachana na jembe la mkono.

Mbunge huyo aligawa katika vijijini 20, kati ya 68 vinavyounda jimbo hilo, huku akijipanga kuendelea zaidi hapo baadaye ili kuhakikisha wakulima wote jimboni wanatumia jembe la kukokotwa na ng'ombe.

"Tumeanza rasmi kampeni za kuachana na jembe la mkono ikiwa ni mwelekeo wa kwenda kwenye trekta, lakini tunaanzia plau kwanza, ambazo nimegawa katika vijiji 20," anasema Profesa Muhongo.

Alipotoa msaada wa plau, kuna utaratibu wa kukopa matrekta unaoendelea ambao unaandaliwa na Idara ya Kilimo ya Halmashauri ya Musoma, kwa ajili ya vyama vya ushirika vya msingi vilivyopo.

"Musoma Vijijini lina jumla ya vyama 35 vya ushirika vya msingi vya ushirika na halmashauri iko tayari kuvisaidia kutayarisha nyaraka za kutafuta mikopo ya kununulia matrekta kwa manufaa ya wanachama," anasema.

Inajulikana, plau zina uwezo wa kulima eneo kubwa kwa muda mfupi kuliko jembe la mkono, hivyo hatua ya wakulima kugawiwa majembe hayo, itasaidia kuwarahisishia shughuli za kilimo.

Majura Mbogora, ni mkulima wa kijiji cha Bukumi, anayesema, kwa kutumia plau, anaweza kulima ekari moja kwa siku moja badala ya siku tano hadi saba, ambazo anatumia jembe la mkono.

Anasema, kupatikana kwa majembe ya kukokotwa na ng'ombe ni mojawapo ya hatua muhimu kwa ajili ya kupanua ukubwa wa mashamba yao ambayo watayalima kwa kutumia muda mfupi.

# Lukuvi atumbua kigogo NHC

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameeleza kutoridhishwa na utendaji kazi wa Kaimu Mkurugenzi wa Miliki wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Grayson Godfrey. Lukuvi jana Dar es Salaam alimvua cheo mkurugenzi huyo, baada ya kugundua uzembe kazini na kusababisha upotevu wa fedha za serikali kutokana na moja ya nyumba za shirika kupangishwa kinyume cha utaratibu wa shirika hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari Lukuvi alimwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Maulid Banyani, kumwondoa Godfrey katika nafasi hiyo na kuangalia wote waliohusika au kushiriki kwa upotevu wa fedha hizo kuchukuliwe hatua za kinidhamu. Alisema amepata taarifa kuhusu kuwapo kwa mpangaji Safina Shabani aliyepangishwa katika moja ya nyumba za shirika hilo, kuhusishwa na ukwepaji wa kodi kwa muda wa miaka 13. "Amekuwa akipoteza kodi ya serikali kiasi cha Sh. 470,000 kila mwezi, hali inayoonyesha kuwapo kwa uzembe mkubwa unaoendelea," alisema Lukuvi. Aliongeza kwamba mkurugenzi huyo amekuwa mzembe hadi kupelekea kupoteza pato la taifa zaidi ya Sh. milioni 6.1 kuanzia mwaka 2006 hadi sasa.

Aidha, alimwagiza Bayani kumtafuta mpangaji huyo na kumnyang'anya umiliki wa nyumba hiyo ya shirika na kumtaka alipe kodi aliyoiibia serikali.

# Sheikh Mkoa aongoza mazishi bosi Zam Zam

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHEIKH wa Mkoa wa Dodoma, Rajabu Mustapha, ameongoza mamia ya watu katika mazishi ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Zam Zam Islamic, Rashid Bura, anayedaiwa kukutwa amefariki dunia ofisini kwake jijini.

Mwili wa Bura, ambaye kifo chake kimeendelea kuzua utata, ulizikwa jana katika makaburi ya Chamwino jijini.

Inadaiwa kuwa Bura (60), alikutwa amefariki dunia juzi ofisini kwake, lakini bado Jeshi la Polisi halijaeleza sababu za kifo chake.

Akizungumza wakati wa mazishi hayo, Sheikh Mustapha aliwataka waumini kufanya matendo mema kama alivyokuwa Bura kwa kuwaheshimu wakubwa na wadogo. Alisema binadamu hawana budi kufanya matendo mema yanayompendeza Mungu ili wapate thawabu wakiwa hai.

Rafiki wa karibu na mwanzilishi mwenzake wa Taasisi ya Dalai Islamic Center, Abdillah Mboryo, alidai uchunguzi wa tukio hilo unaendelea, lakini walilazimika kufanya maziko kwa kuwa mwili wa Bura ulikuwa umeharibika.

Mboryo alidai mara ya mwisho Bura alionekana Jumapili jioni aliposali katika Msikiti wa Nunge na baadaye aliwanunulia kahawa baadhi ya watu waliokuwa karibu na eneo hilo. "Lakini, baada ya hapo hakuonekana wala simu yake haikupatikana hadi jana, mwili ulipokutwa ofisini ukiwa na majeraha matatu na hakuwa na nguo hata moja," Mboryo alidai.

Alisema kuwa Bura aliwahi kufanya kazi Jeshi la Polisi kitengo cha upelelezi katika mikoa mbalimbali na aliwahi kuwa mlinzi eneo la Ikulu kwa miaka mitatu katika utawala wa awamu ya kwanza.

# Watoto 40 wazaliwa mkesha Krismasi

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATOTO 40 wakiwamo wa kike 23 na wa kiume 17 wamezaliwa katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma katika Mkoa wa Lindi mkesha wa sikukuu ya Krismasi na 'Boxing Day'.

Vituo hivyo ni Hospitali ya Nyangao, Sokoine na Kituo cha Afya cha Manispaa ya Lindi, Hospitali ya Kipatimu, Wilaya ya Kilwa na Ruangwa, huku za Wilaya ya Liwale na Kinyonga iliyopo Kilwa, idadi yake hazikupatikana kufuatia wahusika wake kutopokea simu na wengine kuzimwa walipopigiwa.

Kwa mujibu wa wanganga wa zamu katika hospitali za Nyangao, Sokoine, Nachingwea, Ruangwa na Kituo cha Afya cha Manispaa ya Lindi, watoto hao walizaliwa usiku wa Desemba 24 kuamkia Desemba 25 na 26 Siku ya Zawadi (Boxing Day).

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Dk. Francis Msagati wa Nyangao, alisema watoto waliozaliwa ni tisa katika hao wa kike sita wa kiume watatu, huku mmoja akizaliwa kwa njia ya upasuaji.

Dk. Mmuni wa Hospitali ya Sokoine alieleza kuwa watoto waliozaliwa ni sita, kati yao watatu wa kike na watatu wa kiume, na kwamba wakati mmoja akizaliwa kwa upasuaji.

Dk. Abdull Said wa Kituo cha Afya Lindi Manispaa, alisema watoto wliozaliwa ni wawili, wote wa kike. Naye Dk. Regina Ruambo wa Hospitali ya Kipatimu Wilaya ya Kilwa, alisema waliozaliwa ni watoto wa kiume wawili, mmoja akizaliwa kwa njia ya upasuaji.

Naye Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Ruangwa, Dk. Mahela Njile, alisema waliozaliwa ni watoto nane, kati yao wa kike watatu na kiume watano, kati ya hao watatu wakiwamo wawili na wa kike mmoja walizaliwa kwa njia ya upasuaji.

Dk. Salma Litanda wa Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea, alisema watoto waliozaliwa ni 13, ambapo tisa ni wa kike na wanne wa kiume. Alisema mama mmoja alijifungua mapacha.




# Barabara yaongeza kasi kubwa biashara bandarini

**Na Elizabeth Zaya, RUKWA**

KUKAMILIKA kwa barabara kutoka Tunduma kupitia Sumbawanga hadi Bandari ya Kasanga mkoani Rukwa kumeanza kuongeza kasi ya biashara katika bandari hiyo.

Wakizungumza katika Bandari ya Kasanga iliyopo katika Wilaya ya Kalambo mkoani humo, madereva wanaosafirisha saruji kutoka mkoani Mbeya kupeleka katika bandari hiyo ya Kasanga, walisema kwa sasa wanatumia muda mfupi kufika bandarini hapo tofauti na ilivyokuwa awali.

Walisema kutokana na kutumia muda mfupi, kumechangia kufanya safari nyingi na kuongeza idadi ya mzigo katika bandari hiyo ambao unasafirishwa kwa njia ya maji kupelekwa nchi jirani.

Charles Masikini, anayesafirisha saruji kutoka Mbeya hadi bandari hiyo, alisema walikuwa wanasafiri kuanzia siku nne hadi saba kabla ya kutengenezwa kwa barabara hiyo, lakini kwa sasa wanatumia siku moja tu.

Pia alisema kwa sasa wameongeza idadi ya safari na kwamba kwa wiki moja wanafanya safari sita kutoka moja ya zamani kabla ya kutengenezwa kwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Pia alisema kipato chao kimeongezeka zaidi na hawapati hasara kama awali.

Elias Sadala, ambaye naye ni dereva wa gari zinazosafirisha saruji alisema kabla ya kutengenezwa barabara hiyo walikuwa wanalazimika kulala njiani siku nyingi, hivyo kuishiwa akiba ya pesa na hata kusababisha migogoro kwenye ndoa zao.

"Yaani tunaishukuru sana serikali kwa jitihada hizi, tunafurahia kazi yetu kwa sasa, kikubwa tunachoomba kwao watuongezee meli katika Bandari yetu hii ya Kasanga, kwa maana mizigo sasa hivi ni mingi, tunaipongeza pia TPA (Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania) kwa kutuboreshea mazingira ya bandari yetu, inaonekana ya kisasa tofauti na zamani," alisema Sadala.

"Tunaomba na vyombo vinavyohusika na usafirishaji katika barabara ya Tunduma vishughulikie tatizo la msongamano wa foleni katika eneo hilo, tunashukuru shida hii imeisha katika maeneo mengine, ni pale tu ambapo panatuchelewesha sana."

Nahodha wa meli ya Rwegula ya nchini Burundi ambayo inachukua mzigo kutoka katika Bandari ya Kasanga kupeleka nchini humo, Bonyumuvunyi Michael, alisema maboresho yanayofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) katika bandari hiyo yameongeza kasi ya biashara.

Alisema kabla ya maboresho hayo walikuwa wanachukua muda mrefu kwa kusubiriana kupakua mzigo, lakini kwa sasa meli mbili zinapakua kwa wakati mmoja.

Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Percival Salama, alisema Bandari hiyo ya Kasanga ni ya kimkakati kwa ajili ya kuimarisha biashara katika nchi za Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kuongeza uchumi wa Tanzania.



Wafagiaji wa barabara ya Mwananyamala eneo la Kwa Mama Zakaria jijini Dar es Salaam wakiongoza magari yapite kwa urahisi jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kifo mjamzito, mwanawe mtoni chaibua kinamama

**INATOKA UK. 3**

hali ambayo ni hatari kwani hawawezi tena kuvuka kwa kuwa hawana uhakika kama daraja hilo bado lipo au linakuwa limesombwa na maji.

Naye Rozimary Simzosha, alisema hofu pia huwa kwa watoto wao ambao wamekuwa wakivuka kivuko hicho ambacho ni hatari, kwa kuwa kimetengenezwa kwa miti, hivyo kuteleza hali inayosababisha baadhi yao kutumbukia mtoni na kufa maji.

"Kivuko hicho kimetengenezwa kienyeji sana na miti ikilowana maji inateleza, hivyo ni rahisi hata kwa binadamu kuteleza na kuangukia ndani ya maji na kupoteza maisha. Tunaiomba serikali ione umuhimu wa kutujengea daraja ili kunusuru maisha yetu," alisema. Akizungumzia tukio hilo mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Nobert Mwanawima, alisema mjamzito hiyo na mtoto wake walikufa maji kutokana na eneo hilo kutokuwa na daraja la kuvukia, hivyo wananchi wa kijiji hicho kutengeneza kivuko cha miguu kinachokatisha mto kwa kutumia miti.

Alisema mwanamke huyo alipokuwa akipita katika kivuko hicho pamoja na mwanaye waliteleza na kuangukia mtoni kisha walianza kupiga kelele za kuomba msaada, lakini kwa kuwa watu walikuwa mbali hawakufanikiwa kufika kwa wakati kuwasaidia.

"Siku mbili baadaye walipata taarifa kuwa miili yao ilipatikana katika kijiji jirani, na wakazi wa kijiji hicho baada ya kuona kuwa watu hao hawafahamiki waliamua kufanya maziko, ndipo walipoamua kuchukua msiba na kuusafirisha hadi kijiji cha Katete walipokuwa wakiishi," alisema.

Diwani wa kata hiyo, Richad Kamagari, alisema matukio ya watu kutumbukia mtoni yamekuwa yakijitokeza mara nyingi, na yeye ameshatoa taarifa katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo.

Kwa upande wake, Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Kalambo, Mahmood Shauri, alisema serikali itajitahidi kutatua changamoto hiyo inayowakumba wakazi wa kijiji hicho.

## Abiria wakoshwa treni Dar-Moshi

**INATOKA UK. 3**

kusitishwa kwa miongo miwili na nusu.

Alisema huduma hiyo imesaidia kupunguza adha ya usafiri kwa wananchi, ikizingatiwa ni utamaduni wa wazaliwa wa Kilimanjaro kurejea nyumbani mwishoni mwa mwaka.

Alisema huduma inayotolewa katika usafiri huo ni nzuri na nauli zake ni himilivu, akisifu uongozi kwa kuweka kiwango kinachoendana na hali halisi ya maisha ya Watanzania walio wengi.

"Nauli ni Sh. 10,700 kwa daraja la tatu, Sh. 15,300 daraja la pili la kukaa na 25,400 la pili la kulala," Lyimo alibainisha.

Aliongeza kuwa miaka ya nyuma, kipindi kama hiki, kiwango cha nauli ya mabasi kilikuwa kinapanda kutoka Sh. 25,000 hadi 38,000 kwa kila abiria, hivyo treni imeokoa fedha zao.

Isack Gaspar, mhudumu katika treni hiyo, aliwashukuru Watanzania kwa kuwaamini na kutumia usafiri huo.

"Ndani ya treni tunatoa huduma ya nyama choma na vinywaji na tulikuwa tunabeba kreti 50 za vinywaji ila kwa sasa tunachukua zaidi ya 150, kutokana na idadi ya abiria kuwa kubwa," alisema.

## Uwekezaji kadi za kielektroniki sasa watajwa kukuza uchumi

**INATOKA UK. 3**

msukumo mkubwa kwa wawekezaji wa kiwanda cha DZ Cards Afrika kupanua masoko zaidi," alisema.

Matumizi ya kadi za kielektroniki ni muhimu katika uchumi kwa husaidia kupunguza vitendo vya rushwa na kuongeza uwazi katika ukusanyaji wa mapato ya nchi.

Kiwanda cha DZ Cards Afrika kilianza uzalishaji miaka minne iliyopita na tangu wakati huo kimepata wastani wa mauzo ya Dola za Kimarekani milioni 2.9 (zaidi ya Sh. bilioni 6.67).

Kiwanda hiki huzalisha kadi mbalimbali na zenye viwango vya kimataifa zinazotumika kufanya miamala katika sekta mbalimbali za uchumi. Baadhi ya kadi hizo ni 'Mastercard' na 'Visacard'.

Alisema kiwanda cha DZ Cards Afrika kitakuwa na uwezo wa kuajiri zaidi ya watu 400, wakati uzalishaji ukiwa katika kiwango cha juu. Kwa sasa kinaajiri watu 100.

Kwa sasa kiwanda hicho kinafanya uzalishaji wa ziada ili kusaidia kiwanda mama cha DZ Cards kilichopo Thailand kufikia mahitaji makubwa ya kadi ya kielektroniki kwa wateja wake.

Teknolojia ya DZ Card iligunduliwa mwaka 1971 na Jø rgen Schmidt na baada ya hapo iliendelea kukua na kusambaza viwanda vya kutengeneza kadi za kielektroniki sehemu kadhaa duniani ikiwamo Tanzania.



Wakazi wa Tandale, Dar es Salaam wakivuka kwa tabu daraja linalounganisha Tandale na Kwa Ali Maua, baada ya kujaa maji yaliyokuwa yanatoka eneo la Manzese jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Mkandarasi aahidi kasi ujenzi hospitali

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

MKANDARASI wa ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini unaojengwa mkoani Mtwara ambaye ni Shirika Nyumba la Taifa (NHIC), amesema kuwa atahakikisha anafanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha ujenzi huo kama mkataba unavyotaka.

Kauli hiyo ilitolewa na Meneja wa Shirika hilo Mkoa wa Mtwara, Angelina Magazi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye eneo la ujenzi huo wakati wa kuangalia maendeleo ya ujenzi.

Alisema wanatambua kuwa serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 15 kwa ajili kujenga hospitali hiyo ili kupanua wigo wa utoaji huduma za afya hasa kusini.

Magazi alisema wao kama makandarasi wa mradi huo mkubwa hawataiangusha serikali, hivyo watafanya kazi usiku na mchana ili hospitali hiyo ikamilike kwa wakati.

Alisema kazi hiyo imefikia asilimia 20, lakini kasi ya ujenzi huo imekuwa kubwa hivyo kuna matumaini makubwa ya kukamilika kama mkataba unavyotaka.

Magaza alisema kwa mujibu wa mkataba ujenzi wa hospitali hiyo, unatakiwa kukamilika Julai Mosi 2020 na kutoa huduma kwa wananchi.

"Tumejipanga kufanya kazi kwa saa yote 24 iwe mchana au usiku tunafanya kazi hakuna kulala lengo kazi hii ikamilike kama tulivyokubaliana katika mkataba," alisema Magaza.

Alieleza kuwa watahakikisha majengo yote yanajengwa katika ubora unaoendana na thamani halisi ya fedha za serikali zilizotolewa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Evodi Mmanda, alisema serikali imefarijika na kasi ya ujenzi huo.

Alisema kila wakati wamekuwa wakitembelea eneo la ujenzi wa hospitali hiyo, na ni wazi kuwa jinsi kasi ya ujenzi ilivyo ni matumaini kuwa ujenzi utakamilika kwa wakati.

"Tutasimamia kwa uhakika na kufika kila wakati kuangalia jinsi ujenzi huu unavyotekelezwa, lakini hadi sasa tumefurahia kasi ya ujenzi na mradi huu utakamilika vizuri," alisema Mmanda.

Alisema kukamilika kwa mradi huu wananchi wa mkoa wa Mtwara watanufaika na huduma bora za afya.

# Wasaidizi wa kisheria wapewa angalizo

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MKURUGENZI wa Taasisi ya Kawiye Social Development Foundation, Ezekiel Kasanga, amewataka wasaidizi wa kisheria mkoa wa Simiyu waliopata mafunzo ya msaada wa kisheria kutojiita wanasheria.

Lasanga amewaeleza wasaidizi hao kuwa kufanya hivyo ni kukiuka sheria ya msaada wa kisheria.

Kasanga alisema hayo jana wakati wa kufunga mafunzo ya wiki mbili kwa wasaidizi wa kisheria 31 kutoka wilaya zote za Mkoa wa Simiyu.

Alisema hakuna kitu kitakachofanyika bila kufuata sheria na taratibu za nchi, hivyo ni vizuri wakaenda kufanya kazi zao za usaidizi wa kisheria kama walivyofundishwa, na sheria inavyowatambua.

Kasanga aliwataka kufanya kazi ya usaidizi wa kisheria kwa uadilifu na kuwasaidia wenye uhitaji wa kisheria hususan wanawake na watoto ili waweze kupata haki zao wanazozikosa.

"Ninawaombe mkafanye kazi ya usaidizi wa kisheria kwa kufuata taratibu zinazotakiwa... uadilifu ndio kitu pekee ambacho kitawafanya mfurahie utendaji wenu wa kazi, huku mtambue kazi ya usaidizi wa kisheria ni ya kujitolea...haina malipo na kamwe msiombe wala kupokea rushwa," alisema.

Naye Mwanasheria Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mwanahamisi Kawega, aliwasisitiza wasaidizi hao kufanya kazi kwa kuzingatia sheria na kutoa ushirikiano katika vyombo vya serikali kama Polisi, Mahakama na Takukuru ili wawe na dhumuni moja la kumsaidia mwananchi anayekosa haki yake ya msingi.

Baadhi ya wasaidizi hao waliopatiwa mafunzo ya usaidizi wa kisheria, walisema kupitia mafunzo hayo watasaidia jamii kubwa zaidi inayowazunguka kupata haki zao pamoja na kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Sarah Maduka, kutoka Kata ya Somanda Halmashauri ya Mji wa Bariadi, alisema kumekuwapo na uonevu mwingi katika maeneo wanayoishi na kusababisha haki za wahusika kukosekana.

# Agizo la DC latesa kampuni za ulinzi

**Na Said Hamdani,** LINDI

BAADHI ya taasisi zikiwamo za umma kuchelewesha utoaji malipo kwa huduma za ulinzi wanazopatiwa na kiwango kikubwa cha mishahara inayotakiwa kulipwa kwa wanaotekeleza kazi hiyo, imetajwa kuwa ni changamoto inayochangia kampuni za ulinzi Wilaya ya Lindi kuajili walinzi wasiopitia aina yeyote ya mafunzo.

Hayo yalielezwa na baadhi ya wamiliki wa kampuni za ulinzi mkoani Lindi walipozungumza na wanahabari wakati wa ufungaji mafunzo ya tisa kwa wahitimu wa mgambo wa Manispaa ya Lindi.

Baadhi ya wamiliki waliohudhuria ufungaji wa mafunzo hayo, walitoa malalamiko hayo kufuatia agizo lililotolewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Shaibu Ndemanga, kuwataka wamiliki wote wa kampuni za ulinzi Wilaya ya Lindi kuajili walinzi waliopitia mafunzo ya uaskari na si vinginevyo.

Ramadhani Rashidi Chipyangu, anayemiliki kampuni ya Mwene Security Services Ltd na Shani Said (Twiga Securty) walisema wapo tayari kuajiri walinzi waliopitia mafunzo ya uaskari, lakini mazingira si rafiki kutokana na viwango vikubwa vya mishahara wanayohitaji.

Mazingira mengine waliyoyataja ni walinzi waliopata mafunzo ya uaskari kutokuwa tayari kuvumilia pale malipo yanapochelewa kutoka kwa taasisi wanazozihudumia.

Walisema tunalipa mishahara baada ya wateja wao (taasisi) kuzilipa kampuni zao fedha za huduma za ulinzi walizozipatia.

Walisema kampuni zina utaratibu wake ikiwamo mikataba inayoingia na taasisi za umma na binafsi, hivyo askari kuna mambo anayoyahitaji ambayo kimsingi hayawezi kutekelezwa kama wanavyotaka wao kulingana na hali ya kipato wanachokipata kutokea taasisi husika.

Ally Hassani Bakarim anayemiliki Kampuni ya Haba Security Guard, alisema walinzi 30 alionao wote wamepitia mafunzo, wakiwamo na waliohitimu Desemba 21, mwaka huu, hivyo agizo la kiongozi huyo wa wilaya amelipokea kwa mikono yote miwili.

Akifunga mafunzo kwa askari mgambo 130 katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, Mkuu wa Wilaya hiyo, Shaibu Ndemanga, ameziagiza kampuni zote za ulinzi zinazohudumu ndani ya wilaya hiyo kuwaajiri walinzi waliopitia mafunzo ya uaskari.

# Walalamikia utata malipo ya Tasaf

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

VIONGOZI wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) unaotekelezwa na serikali kuboresha maisha ya wananchi kutoka katika kaya maskini zinazoishi katika mazingira magumu wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, wametuhumiwa kutafuna mamilioni ya fedha za mradi huo.

Taarifa zinaeleza kuwa fedha hizo zilizotafunwa kiujanja na baadhi ya viongozi hao zilitolewa na Serikali Novemba 2018 ili kulipwa kwa walengwa, badala yake zikaishia mifukoni mwa viongozi hao.

Inadaiwa kuwa fedha hizo zilipangiwa kufanya kazi ya kuwalipa posho wanakamati ambao walisimamia shughuli za ajira za muda uliobuniwa na kutekelezwa na Tasaf katika kipindi cha Agosti, Septemba na Oktoba 2018 ikiwa na lengo la kuboresha vipato kwa wananchi wanaonufaika na mradi huo kutoka katika kaya hizo.

Wakizungumza bila kutaja majina yao, baadhi ya wasimamizi hao walisema wajanja hao walikula baadhi ya fedha za malipo ya miezi yote mitatu zilizotakiwa kulipwa kwa wanakamati wa vijiji vilivyopo pembezoni ambavyo ni miongoni mwa vijiji 88 vinavyotekeleza mradi huo.

Baadhi ya wanakamati walidai kuwa maofisa hao wametafuna zaidi ya Sh. milioni 10 kati ya fedha hizo.

Viongozi hao ambao walionyesha baadhi ya nyaraka kutoka katika Ofisi ya Tasaf wilayani humo zilithibitisha kuwa zaidi ya wanakamati 268 kutoka katika vijiji 67 kati ya vijiji 88 vyenye wanakamati 352 vinavyo tekeleza mradi huo hawajalipwa posho zao za mwezi mmoja kila mmoja.

Imedaiwa zaidi kuwa ili kuwafunga midomo baadhi ya wanakamati walilipwa wastani wa Sh. 276,000 kila mmoja wao ikiwa ni malipo ya posho za miezi miwili kati ya mitatu waliyotakiwa kulipwa.

Aidha, imedaiwa kuwa wanakamati kutoka katika tarafa zilizopo maeneo ya mjini wao walilipwa fedha za miezi mitatu yote.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Gasper Balyomi, alipotakiwa kuzungumzia malalamiko hayo alidai kwa vile mradi huo ulitekelezwa wakati ambao hakuwa mkurugenzi wa halmashauri hiyo, hajui na hana taarifa zozote za madai ya kutafunwa kwa fedha hizo.

Haya hivyo, alimuita Mratibu wa Tasaf Wilaya ya Tunduru, Mhidin Shaibu, ambaye alikiri kutolipwa baadhi ya wanakamati hao kutokana na fedha zilizoletwa katika kipindi hicho kutotosheleza na kwamba baada ya kukamilika kwa taratibu za malipo hayo ya awali ofisi yake ilipeleka taarifa Tasaf makao makuu, na madokezo ya madai yao yameshafanyiwa kazi kinachosubiriwa ni kuingiziwa fedha ili waweze kuwalipa.

Alisema ili kuondoa malalamiko hayo ofisi yake inafanya utaratibu wa kupita katika maeneo ya vijiji husika na kufanya mikutano ya kuwataarifu namna taratibu za madai yao zinavyoendelea kufanyiwa kazi ikizingatiwa uwapo wa mabadiliko ya taratibu zinazotakiwa kufutwa kabla ya kuingiziwa fedha hizo.



Fundi wa rangi akipaka rangi kwenye nguzo zilizopo katika daraja linalounganisha Mwananyamala kwa Manjunju na Tandale jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanawake wawezeshwa kwa vyerehani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya wanawake 30 wa Kata ya Isaka Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wamepatiwa vyereheni na ofisi bure vyenye thamani ya Sh. milioni 15 na Jumuiya ya International Istaqaama Muslimu Community ili kuondokana na adha ya kuendelea kukodisha vyerehani kwa Sh. 15,000 kwa siku.

Akikabidhi vyerehani hivyo kwenye mradi wa ushonaji wa kinamama wa Ki-ibadhi Kata ya Isaka, Mzee wa Jumuiya ya Waibadhi wa Kahama, Mohamed Maliki, alisema vyerehani vilivyotolewa vitumike na wanawake wote wa Isaka bila kujali imani za kidini.

Maliki alisema vyerehani vilivyotolewa vinatakiwa kuwanufaisha wanawake wote wa kata hiyo, bila kujali dini na itapendeza zaidi kama wanafunzi watakaokuwa wamehitimu elimu ya msingi na sekondari waweze kujifunza ufundi kupitia vyerehani hivyo.

"Tunataka vyerehani hivi tulivyotoa viweze kuwanufaisha wanawake wote wa kata hii ya Isaka na kata za jirani bila kubaguana...Tungependa kuona mradi huu unawanufaisha pia wanafunzi wakike na wa kiume waliohitimu elimu ya msingi na sekondari," alisema Maliki.

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Isaka, Rajabu Rashidi, aliwapongeza wafadhili kwa kutoa vyerehani hivyo kwa ajili ya kinamama na kuwaondolea changamoto ya ukodishaji wa cherehani ambayo ilikuwa ikiwafanya kushindwa kufanyakazi kwa uhuru na ufasaha.

Katibu wa Kamati ya Masjidi ya Alwahaab, Ahmed Harouni Alnoobiy, alisema mradi huo ufike sehemu waume zao watakapo legalega kiuchumi kwenye familia waweze kuwasaidia kimajukumu na kuwataka kutunza vyerehani visije vikaharibika.

# Wanaokimbia ukeketaji kuwezeshwa zaidi

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Hope for Girls and Women Tanzania, linatarajia kupanua shughuli za kituo chake cha nyumba salama kilichopo mjini Mugumu Serengeti Mara, kwa kuanzisha ufugaji, kilimo hai na madarasa ya ufundi.

Shirika hilo pia linatarajia kujenga hosteli na maktaba, lengo likiwa ni kuwapa ujuzi mabinti hao, ili wanapotoka katika nyumba salama wawe wana ujuzi wa kuwezesha kujitegemea.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Rhobi Samwelly, alisema wana eneo la ekari 20 nje ya mji wa Mugumu, walilonunuliwa na mmoja wa wafadhili wao aliyemtaja kwa jina la Singita Grunet.

"Tunataka kupanua shughuli za kituo kwa kuweka majengo yakiwamo ya hosteli, madarasa ya ufundi, kilimo hai, ufugaji na maktaba, tayari tuna Sh. milioni 72 za kuanzia tulizopewa na watu wa Canada," alisema Rhobi.

Rhobi alisema, eneo ambalo nyumba salama ipo kwa sasa ni finyu, hali inayosababisha kuwa na mabweni yenye upana madogo ikilinganishwa na idadi ya mabinti waliopo.

Alisema, madarasa pia ni machache, hali inayolazimu masomo yote kufundishwa sehemu moja na kuwanyima wanafunzi wa ufundi sehemu ya karakana kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

Aliongeza kuwa kuna upungufu wa eneo la kuweka vitanda vya ziada, na wanaomba kupata ufadhili utakaofanikisha ujenzi wa makazi yao ya kudumu eneo la Matare ambako wana ekari 20.

"Kwa sasa kuna mabinti 67, wengine walisharudi kwa wazazi wao baada ya kujenga uhusiano mzuri, lakini tunaendelea kupokea wapya, kwa sababu vitendo vya ukeketaji vipo, hivyo ni muhimu kupanua shughuli zetu," alisema.

Alisema nyumba salama ni kimbilio la wasichana wengi wanaopokelewa hapo na kujifunza ufundi, ujasiriamali, kilimo, sheria, Kiingereza, hisabati, masomo ya kawaida ya kimtaala, kuhusu madhara ya ukeketaji na afya ya uzazi.

Kadhalika alisema, wanajifunza stadi mbalimbali za kilimo na ufundi na kupata utaalam wa kutengeneza vikapu, sabuni za maji, kushona mikoba, mabegi na nguo za mitindo mbalimbali.

Alisema, wakifanikiwa kujenga nyumba salama kwenye eneo letu la ekari 20, ana uhakika shughuli zao za kuwasaidia wasichana na watoto wanaokimbia ukeketaji zitafanyika kwa ufanisi zaidi.

Shirika hilo limekuwa likiwezeshwa na wafadhili mbalimbali wakiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA) na Four Seasons Serengeti.

# Magendo mifugo yainyima serikali mapato

**Na Mwandishi Wetu,** LONGIDO

SERIKALI imekuwa ikipoteza mapato ya kati ya Sh. bilioni nne hadi tano kwa mwaka, kufuatia uuzwaji wa mbuzi kwa magendo kupelekwa Kenya.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe.

Alisema serikali imekuwa ikikosa mapato ya Sh. bilioni nne hadi tano kwa kipindi cha miaka mingi kutokana na mifugo hiyo kwenda kuuzwa Kenya, kupitia mpaka wa Namanga.

Hata hivyo, alisema serikali hadi kufikia mwaka jana wamefanikiwa kudhibiti uuzwaji wa mifugo nje ya nchi ili kuokoa fedha zilizokuwa zinapotea.

"Mbuzi walikuwa wakiuzwa kwa njia za magendo na njia halali, lakini njia ya magendo ilikuwa ikiuza mbuzi wengi zaidi, tumechukua hatua kama serikali ya kudhibiti na tumekuwa wakali sana na tumeshaeleweka sasa mambo yanakwenda vizuri," alisema Mwaisumbe.

Alisema ilibidi serikali kuwa wakali ili kurudisha hali ya uhalali wa biashara ya mbuzi na wakati mwingine walikuwa wakitaifisha mifugo iliyokamatwa kutoka kwa wafanyabiashara waliokuwa wakiuza kwa njia za magendo. "Tukikamata mbuzi na kugundua wanauzwa kwa magendo tunawataifisha maana siwezi kuona serikali inakosa mapato kutokana na tamaa za watu wachache, suala hili niko makini naomba wafanyabiashara wanielewe, mapato ndio yanamsaidia Rais John Magufuli katika juhudi zake za kuelekeza Watanzania kwenye uchumi wa kati na kupunguza umaskini," alisema Mwaisumbe.

Hata hivyo, Mwaisumbe alisema ameshawezesha wafanyabiashara hao, kuunda vikundi vya watu kati ya 30 hadi 45 na kuvirasimisha ili kukaa kwa kuangalia mianya ya upotevu wa mapato ya serikali, sambamba na kufanya tathmini ya mafanikio ya wafanyabiashara.

Alisema vikundi hivyo vitawasaidia kuwa na umoja ambao utaunganisha nguvu za pamoja na hata kusafirisha kwa pamoja mbuzi hao, kwa njia halali ili nchi ipate kodi kwa ajili ya maendeleo ya watu wake wakiwamo wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo.

"Tumedhibiti kwa asilimia 90 uuzwaji holela wa mbuzi wa magendo, lakini kwa ushirikiano wa pamoja, wafanyabiashara matarajio yetu ni kufikia asilimia 100," aliongeza Mwaisumbe.




Watoto wakijipiga picha kwa kutumia simu za mkononi maarufu kama 'selfie' katika lango la kuingia Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara jana. Watoto hao walitumia fursa ya sikukuu kutembelea hifadhi hiyo. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Gambo ataka mfumo kidigitali trafiki

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amelitaka Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani mkoani hapa, kutumia mfumo wa kidigitali katika kubaini makosa ya barabarani ili kurahisisha kuwabaini madereva wasiozingatia sheria.

Kauli hiyo aliitoa wakati akizungumza na wadau wa usalama barabarani, askari polisi , wanasiasa na wanafunzi katika kongamano la usalama barabarani lililoandaliwa na kamati ya usalama barabarani Mkoa wa Arusha.

Gambo alisema lazima Mkoa wa Arusha uendeshwe kwa mfumo wa kidigitali kwa kufungwa kamera za kisasa maeneo muhimu ya barabara ili kurekodi matukio mbalimbali ya uvunjifu wa sheria za barabarani na kuweka kumbukumbu za taarifa za dereva wasiozingatia sheria.

"Tuna taarifa watu wanapata leseni kiujanja ujanja bila kupitia vyuo vya udereva na kusababisha ajali ...ni vizuri Jeshi la Polisi likatumia mfumo wa kidigitali kubaini taarifa za madereva wasiotaka kutii sheria," alisema Gambo. Aidha, amelipongeza jeshi hilo kitengo cha usalama barabarani mkoani humo kwa kupunguza ajali za vifo kwa asilimia 10, jambo ambalo linatia moyo, huku akilitaka jeshi hilo, kuweka mkakati wa mwaka ujao wa kupunguza zaidi ajali ili kufikia chini ya asilimia 50.

Pia Gambo ametoa onyo kwa madereva wa utalii wanaosafirisha wageni wakiwa wamelewa ambapo ameliagiza Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua kali za kisheria. Awali Katibu wa Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Arusha, Mary Kipesha, alisema ajali na vifo katika Mkoa wa Arusha zimepungua kwa asilimia 10, huku ajali za majeruhi zikiongezeka kwa asilimia mbili.

Akisema kwa kipindi cha Januari hadi Oktoba mwaka 2019, kulikuwa na ajali 47 zilizosababisha vifo vya watu 32 ukilinganisha na kipindi cha mwaka 2018, ambapo jumla ya ajali 52, zilitokea na kusababisha vifo vya watu 41.

Kipesha alisema tatizo linalosababisha ajali hizo, ni kutokuwapo kwa alama za barabarani, utambuzi wa vituo vya maegesho kwa daladala, machinga kufanyabiashara barabarani na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wa barabara.

Ameziomba mamlaka zenye dhamana ikiwamo Halmashauri ya Jiji la Arusha, Tanroads na Tarura kuweka na kuchora upya alama za barabarani ambazo kwa kiasi kikubwa zimefutika hatua hiyo itasaidia kupunguza ajali zisizokuwa na tija.

Katika hatua nyingine, kamati hiyo ya usalama barabarani imekabidhi gari aina ya Land Cruise V8 Kipesha, kwa ajili ya kusaidia ofisi yake kutekeleza majukumu ya kikazi

# Wazazi wapewa neno kupeleka watoto vyuoni

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WANANCHI wametakiwa kuwapeleka watoto vyuoni kupata elimu ambayo itazalisha wasomi na wataalamu waliobobea wakati nchi ikielekea kwenye uchumi wa kati na viwanda.

Rai hiyo, ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, wakati wa mahafali ya saba ya Chuo cha Veta cha mafunzo ya hotelia na utalii na jumla ya wanafunzi 89 walihitimu.

Muro alisema katika kipindi hiki cha kuelekea uchumi wa viwanda, ni lazima wazazi kuwapeleka watoto vyuoni na baada ya kuhitimu mafunzo watapata ajira ambayo itaisaidia serikali kufikia malengo ya kiuchumi.

"Tatizo linalowakabili wananchi wengi baada ya kuona viwanda na hoteli zimejengwa kwa wingi ndio wanaanza kupeleka watoto vyuoni, na hii imesababisha ajira nyingi katika viwanda na hoteli kuchukuliwa na watu kutoka nchi za nje kwa kuwa wao walijiandaa mapema," alisema Muro.

Alisema serikali imejipanga kuwekeza katika uchumi wa viwanda na mpango huo utasaidia kuzalisha ajira kwa vijana nchini.

Mkuu wa Chuo hicho, Christopher Ayo, alisema chuo hicho kimekuwa kikizalisha idadi kubwa ya wanafunzi ambao wamefanikiwa kupata ajira katika maeneo mbalimbali, pamoja na kujenga mahusiano mazuri na vyuo vya ndani na nje ya nchi hususani vya utalii.

Ayo alisema kupitia ushirikiano huo, wamejenga uwezo mkubwa kwa wafanyabiashara wake hususan wakufunzi na utawala kwa kuandaa mitaala ya mafunzo ya uongozaji wa watalii na utoaji wa huduma.

Alisema chuo hicho kupitia mradi wa ISTEP uliofadhiliwa na Canada, wamenunua vifaa vya utalii vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 63.

Ayo alitaja matatizo yanayokikabili chuo ni upungufu wa kumbi za mihadhara na madarasa, hiyo imetokana na ongezeko la wanafunzi wengi.

"Chuo chetu tumejipanga kukabiliana na matatizo hayo, pamoja na kuongeza udahili wa kufikia 500 kwa mwaka wa masomo," alisema Ayo.

## Walimu wakosa choo wajisaidia zahanati

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WALIMU wa Shule ya Mijongweni, Kata ya Mnadani, Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, hawana huduma ya vyoo kwa zaidi ya miaka 10 hali inawalazimu kujisaidia kwenye choo cha zahanati moja iliyopo jirani na shule hiyo.

Katika kulitafutia ufumbuzi wa kudumu tatizo hilo, tayari halmashauri ya wilaya hiyo imekabidhi mifuko 20 ya saruji, kwa Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mnadani (WEO), Sembuli Mkilaha.

Aliyekabidhi saruji hiyo juzi ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo.

Akikabidhi mifuko hiyo ya saruji, Sintoo alisema kuwa saruji hiyo ni utekelezaji wa ahadi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Hatib Kazungu, ambaye aliahidi kuchangia kwa ajili ya kuanza ujenzi wa choo hicho.

Akipokea mchango huo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mnadani, Mkilaha alimshukuru Dk. Kazungu kwa kutimiza ahadi yake ya kuchangia saruji hiyo kwa ajili ya ujenzi, ambao utatatua kero ya muda mrefu ya kukosekana kwa choo cha walimu.

"Kule kwenye zahanati, walimu wanatumia choo chenye shimo moja tu, jambo ambalo siyo la kawaida kwa huduma hiyo pale inapobidi kutumiwa na hadhira kubwa.

"Walimu waliopo katika shule hii wanatumia choo kimoja kilichopo pale, na wakati mwingine wanapanga foleni kusubiri huduma hiyo kitu ambacho sio kizuri," alilalamika mmoja wa wakazi wa Mijongweni.

Awali, akizungumzia ujenzi wa choo hicho, Mkilaha alisema ujenzi huo unatarajia kukamilika katika kipindi kisichozidi miezi sita na unakisiwa kuigharimu serikali kiasi cha Sh. milioni 16.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa kamati ya shule hiyo, Omari Mgalla, alishukuru kwa mchango huo na kuahidi utaelekezwa katika ujenzi wa choo kama ilivyokusudiwa.



Mtalii kutoka Uholanzi ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini akipiga picha fuvu la nyati, katika eneo la kulia chakula watalii la Msasa lililopo Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara juzi, wakati wa Sikukuu ya Krismasi. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Treni Moshi-Dar mwendo wa bia, nyama choma

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TRENI ya abiria ya Delux inayofanya safari zake kati ya Dar es Salaam na Moshi mkoani Kilimanjaro, imeongeza kivutio kingine cha 'nyama choma' kuuzwa ndani ya usafiri huo baada ya kuwapo kwa huduma ya bia.

Pia huduma ya bia imeongezeka kutoka sanduku 50 hadi 150 kwa siku, kwa wasafiri wanaotoka Dar es Salaam kwenda Moshi.

Jana, mmoja wa wahudumu wa treni hiyo, Issa Gasper alisema hivi sasa wanafanya biashara nzuri, kwa kuwa awali walianza na sanduku 50 za bia na kuisha zote kabla hawajafika Mombo, Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, jambo ambalo liliulazimu uongozi kuongeza huduma hiyo.

"Tuna vinywaji vya kila aina katika treni hii na hakuna kinachobaki kikiingia kwenye treni. Wingi wa abiria hawa ni biashara kubwa kwetu. Tulianza na sanduku 50 za bia zikaisha kabla hatujafika hata Mombo," alieleza Gasper.

Wakati Gasper akisema hayo, juzi Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe alinukuliwa akisema katika treni hiyo inayosafiri usiku, huduma zimeboreshwa na sasa kuna nyama choma na watu wanasafiri raha mustarehe.

Kwa mujibu wa Waziri Kamwelwe, juzi treni hiyo ilipakia abiria 950 kutoka Dar es Salaam kwenda Moshi.

Baada ya kufika katika mji wa Moshi jana asubuhi, mmoja wa wasafiri Emmanuel Kavishe, alisema alikwenda Moshi kwa ajili ya sherehe za mwisho wa mwaka na wanamshukuru Mungu wamefika salama na wapo vizuri.

"Tunamshukuru sana Rais wetu, Dk. John Magufuli kwa kuturahisishia huduma za usafiri, wengi tulikata tamaa ya kuja Moshi, kwa sababu ya uhaba wa mabasi ya abiria, kwa vile gharama za mabasi zilikuwa juu. Leo hata sisi wanyonge tumekuja nyumbani kufurahi na wazazi na ndugu jamaa na marafiki, ni miaka mingi hatukuja maana tulikuwa tukitafuta maisha huko mikoani," alisema Kavishe.

Abiria mwingine wa treni hiyo, Vivian Uisso alisema, "Tumekuja kuungana na wazazi wetu kusherehekea Sikukuu za Krismasi na Mwaka mpya. Sherehe hizi zinaleta umoja, kushirikiana kati ya sisi wenyewe na kuinuana kiuchumi au kibiashara kwa sisi Wachaga. Rais Magufuli Mungu ambariki kwa kitu hiki alichokifanya cha kufufua reli ya Moshi na kurejesha treni ya abiria."

# Watoto wachanga wadaiwa kukeketwa kisiri

**Na Godfrey Mushi**, SIHA

SHUGHULI za ukeketaji wa watoto wachanga, zimeanza kufanyika tena kwa usiri mkubwa katika Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, baada ya mangariba kudaiwa kubuni mbinu mpya ya kukeketa watoto hao wakati wa sherehe za ubatizo.


Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Siha, Marko Masue, alisema hivi sasa wanafanyia kazi uchunguzi wa taarifa za jamii za wafugaji kukeketa watoto wachanga na kuunganisha sherehe hiyo na matukio ya ubatizo wa watoto.

"Tunazo taarifa kwamba huko kwenye maeneo yanayokaliwa na jamii za wafugaji, shughuli za ukeketaji zimeanza tena kwa usiri mkubwa, hasa unaposikia matukio kama ubatizo wa watoto umefanyika kwa wale wakristo, basi ujue mambo tayari. "Tumeanza kukusanya taarifa za uchunguzi na nina amini kuundwa kwa Jukwaa la Ukombozi wa Mwanamke Kimapinduzi (Tapo) kwa Wilaya yetu ya Siha, tutawajua watu hawa na kuwafichua hadharani wanaofanya kazi hiyo, lakini na sisi wa serikali tutachukua hatua ya kuwakamata." Maeneo yanayotajwa zaidi kufanyika matukio hayo ni Kata za Ormelili, Songu, Makiwaru, Donyo, Biriri, Karansi, Gararagua, Mitimirefu, Ndumeti na Ngarenairobi.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Utafiti wa Hali ya Afya na Demografia Tanzania (TDHS) ya mwaka 2015/16, Mkoa wa Kilimanjaro unaripotiwa kuwa na asilimia 10 ya matukio ya ukeketaji. Kuhusu ukeketaji unaoendelea dhidi ya watoto, Wakili Dorice Kinyoa alipotafutwa kutoa ufafanuzi wa kisheria kuhusiana na makosa hayo alisema: "Kosa la ukeketaji, sheria imetamka wazi kwamba adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 15 na faini isiyozidi Sh. 100,000, lakini mkosaji anaweza kuamuriwa kulipa fidia kwa mwathirika."

Awali, akizungumza baada ya kauli hiyo ya serikali, Mratibu wa mradi ujenzi wa nguvu ya pamoja ya kutetea wanawake na watoto wa Mkoa wa Kilimanjaro, Veronica Ullomi, alisema hivi sasa wanaendelea kutoa elimu ya jinsi ya kuwakagua watoto, watoe taarifa kama kuna matukio ya ukatili.

"Ni kweli sisi Shirika la Kwieco, ndio tuliounda Jukwaa la Tapo ili kupambana na ukatili Siha na wanawake hawa watakuwa ni wawakilishi wa wanawake wengine na watatumika kuwaelimisha wanawake wengine kwenye ngazi ya chini zaidi," alieleza Ullomi.



Ukurasa 14

Namna ya kumudu Krismasi na mzigo Januari kwa bajeti



Ukurasa 18

Simulizi inayotoa chozi atoayo binti maskini wa kutisha

BUFE

Ijumaa Desemba 27, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 15

## Krismasi biashara midoli 'haishikiki'



# Chuo Kikuu Bugando wafurahia siku yao wakipanda miti watakapohamia

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

NI wiki moja kabla, Hospitali ya Kanda Bugando ilifanya sherehe ya kuadhimisha siku yao katika kiwanja cha Nyamagana jijini hapa. Waalikwa wa karibu, walikuwa pacha wao kikazi, Chuo Kikuu cha Katoliki cha Sayansi ya Tiba za Afya ya Binadamu (Cuhas) Bugando. Ilinoga sana!

Baada ya wiki moja, pacha hao ambao wamejikita katika kuandaa wataalamu wa afya ya matibabu nao wakawa na tukio la aina hiyo. Nayo ikafana sana, ikiwa na waalikwa pacha wao kutoka hospitali ya Bugando.

Vyote katika sura inayofanana, sherehe iliyotangulia ya hospitali, ikafuatwa na chuo, zimesheni ratiba zenye matukio mengi ya kufurahisha, ikiwamo michezo ya kuburudisha washiriki mbalimbali na wafanyakazi waliojumuika kikazi, baadhi yao ni bao na drafti.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Neema ya uchumi wa kisasa kwa wanaokimbia shida ukeketaji

Ukurasa 20

UCHUMI

# Namna ya kumudu Krisma mzigo Januari kwa bajeti s

- Mtaalamu adokeza pa kukanyaga, kukwepa
- Mambo nane nyeti yanayonyoosha sikukuu



Ndivyo ilivyo katika pilika pilika za kununua nguo na bidhaa zingine kwa ajili ya Krismasi, siku chache kabla ya kuwadia. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

JUZI Jumatano watu wote duniani walisherehekea Krismasi, sherehe ya kuzaliwa mwokozi wao, Yesu Kristo. Namna ya kusherehekea na yatokanayo na sherehe hizo yana mengi.

Iko wazi kwamba, kuna kundi kubwa ni la wafanyakazi na wasio wafanyakazi ama wako likizo au walau mapumziko mafupi ya kusherehekea. Vivyo hivyo, kuna hatua mbalimbali za kipekee kwa mwaka zinachukuliwa ndani ya maisha ya jamii. Jibu mojawapo kubwa ni kwamba, kuna pesa inayotumika.

Pia katika sura ya pili, sikukuu hiyo inaendana na wiki moja baadaye, kuwapo na mapumziko ya siku ya Mwaka Mpya, kisha 'kitu' kinachofuata ni wazazi wenye watoto shule wanajiweka sawa kugharamia mahitaji ya huko. Hutajwa 'si mchezo'.

**KANUNI X- MAS**

Kwanza kabisa, Krismasi inapotimu, ambayo kwa uhalisia wa sasa ilikuwa juzi, mtu anatakiwa kuhakikisha anatumia muda huo kufurahia kadri ya uwezo wake, lakini asitumie fedha asizo nazo mfukoni.

Wataalamu wa kifedha na uchumi binafsi, wanasema kama mtu alitenga fedha kwa ajili ya sherehe ya Krismasi na Mwaka Mpya, anakuwa na uwezo wa kufanikisha usherehekeaji huo.

> **"Wataalamu wa kifedha na uchumi binafsi, wanasema kama mtu alitenga fedha kwa ajili ya sherehe ya Krismasi na Mwaka Mpya, anakuwa na uwezo wa kufanikisha usherehekeaji huo.**

"Hii ni safari," anaieleza mshauri wa masuala ya fedha, ambaye ni Mwenyekiti na Mwanzilishi wa Taasisi ya Centonomy, mama Waceke Nduati, wa nchini Kenya.

Lakini, inakuwaje baada ya msimu wa sherehe, watu wanasalia na madeni na kufikia hatua ya kuuza au kuweka rehani vitu vyao vya thamani, wamudu kujikimu katika mwezi unaofuata Januari?

Waceke anafafanua: "Tatizo linakuja pale unafanya uamuzi dakika za mwisho kuhusu mipango ya sherehe ambayo hukuwa nayo."

Mtaaluma huyo anaongeza kuhusu kinachotawala fikra za wengi kwamba: "Watu wanakurupuka dakika za mwisho kufanya mipango ya sherehe na kutumia fedha zao kiholela."

Kuna swali lingine, je, unawezaje kusherehekea bila ya kuwa na hofu kutumia fedha ambazo hukuzipangia?

Mama Waceke ana majibu yenye ushauri kwamba, ni vyema kwa mtu akaelewa maana halisi ya Krismasi na maandalizi yanayohitajika.

Kwa mtazamo wake, anasema Krismasi inahusu kusherehekea na watu uwapendao na kuna njia nyingi sana za kufanya hivyo, bila ya kujiingiza kwenye madeni yanayoweza kuepukika.

Pia anaongeza kwamba ni wakati mzuri wa kusoma kitabu, kujifunza kitu kipya kama vile mapishi, ili mradi hicho kinaweza kuepusha gharama zisizokuwa na maana, kama vile kwenda maeneo ya burudani kutumia fedha zisizokuwa katika bajeti.

Mama Waceke, anashauri mtu asichukue deni kwa ajili ya kusherehekea Krismasi, kwani ni kukaribisha tatizo.

**BAJETI INAVYOTENGENEZWA**

- Ujihoji kiasi gani cha pesa kitatumika?
- Kuorodhesha watu unaotaka kuwapa zawadi.
- Tumia pesa ulizotenga kununua zawadi hizo.
- Lipia kila unachotaka kununua kwa pesa tasilimu usikope.

"Watu wengi hujikuta katika madeni kutokana na sababu wanataka kushindana na wenzao, kwa mfano kama jirani yako anaenda kujivinjari Dubai, usidhubutu kushindana na mwenzako, kwa sababu hujui anakotoa fedha zake," anasema Waceke.

Mama huyo anaendelea, kwamba mtu anapaswa kujielewa uhusiano wake na fedha, hoja kuu ni namna gani kiasi cha akiba unaweza kuhifadhi.

**KABLA KUSHEREHEKEA**

Mwezi Januari unapoingia, inaelezwa ni vyema kuzingatia vidokezo kadhaa:

- Tenga fedha za kugharamia huduma zote muhimu kama vile kodi ya nyumba, karo ya shule na chakula.
- Bima ya gari na afya ikiwezekana, lipa moja kwa moja iwapo unahofia kutumia fedha hizo.
- Zitakazobaki, tumia kuwafurahisha watu uwapendao katika maisha yako.
- Kusherehekea sio lazima usafiri, unaweza kuwa nyumbani na watoto wako, ukaamua kuwapikia kitamua wapendacho na kujumuika na familia.
- Jiulize kwa nini natumia pesa hizi zote? Je, nazitumia kufurahisha watu au kujifurahisha?

Mama Waceke, anasema uamuzi na usimamazi wa matumizi muhimu ya Krismasi na Mwaka Mpya hauna tofauti na mtu ananavyosuluhisha uhusiano binafsi na wengine, katika matumizi ya fedha maishani.

**KIKUU DESEMBA 25**

Kuanzia usiku wa kuamkia Krismasi, familia huwa na hekaheka nyingi kufikia siku hiyo, huku katika baadhi ya maeneo ndugu wanaweza kutofautiana kwa kile wanachokitaka kwa siku hiyo, mfano rimoti ya televisheni ya kipi wanataka kuangalia.

Siku chache zilizopita, iliripotiwa nchini Uganda, mume kumzuru mke, kwa kisa cha kumchinja kuku wa sikukuu mapema.

Hivyo, Krismasi inapopangiliwa vizuri, basi sikukuu nayo inakuwa nzuri zaidi. Nini kinafanyika?

Mosi ni upendo wakati wa Krismasi; Kwenda nyumbani mtu alikozaliwa ni huwa jambo la faraja, hata mtu akalala katika kitanda chake cha utotoni anajisikia raha kisaikolojia.

Mtu kama ana ndugu, inakuwa jambo jema kuwa nao karibu kuongea, sambamba na kuwathamini walio karibu yako na kutenga muda kwa ajili yao, vyote vinafanya familia iwe na furaha siku hiyo, hata kama siku kwa saa zote 24.

Pia watu wanapaswa kukubaliana muda wa kufungua zawadi zao, muda wa kula chakula cha mchana au mtu kuendana na mazingira yaliyopo.

Pili sio sikukuu ya upishi peke yake; Upishi wa Krismasi huwa ni

# si na sahihi

shughuli kubwa. Kuna mengi ambayo mara nyingi watu wanatumia ujuzi wote kupika mapochopocho na hekaheka nyingi.

Hata hatua ya kuomba msaada wa jukumu hilo kutoka kwa wengine, kunaelezwa hakuna ubaya, muhimu ni kuwekwa ratiba, ili kila litimie kwa utaratibu.

Ni muhimu katika hilo, kila mmoja akawa na jukumu katika shughuli hiyo.

Tatu Krismasi ni sherehe ya nani? Mara nyingi watu wanaiona sikukuu hiyo ni kwa ajili ya watoto na wengine wanaiona ni ya watu wazima au kuna wakati ni ya familia.

Kadri miaka inavyosonga, ndivyo kuna tofauti zinajitokeza katika sikukuu hiyo.

Watoto wanafurahia kupata zawadi wakati huo, watu wazima wanafurahi vinywaji vya aina mbalimbali kabla ya usiku, ikiendana na mijadala au kijamii, kazi, siasa na burudani. Kikubwa ni kwamba, familia zimeweka utamaduni wa kujumuika kwa pamoja.

Nne, maelewano wakati wa Krismasi; Jamii zinakubaliana kufuata utaratibu fulani ndani ya Krismasi na inakuwa wazo zuri kuleta ili watu waweze heshima kati ya jamii, inayofurahi pamoja bila kukwazana. Anayeudhiwa, hupuuza.

Tano, ni ulingo wa teknolojia; katika hilo kuna kinachotawala katika familia za Kiafrika kwamba, katika ila televisheni moja na wanaoangalia ni wengi.

Hapo ni kwa baadhi 'kukubalia yaishe' katika mtazamo mbalimbali, ikiwamo 'wengi wape' na wennye simu wanazama katika mitandao yao, kama mbadala wa 'plani B.'

Sita, kuna suala la kuimba wakati wa Krismasi; muziki na nyimbo ni namna nzuri ya kufurahia sikukuu na kuileta familia karibu kila mmoja afurahie siku hiyo ya kipekee.

Mtu anaweza kutumia mtindo wa kila mmoja kuimba, ili kuwafanya wajumuike kwa karibu zaidi.

Saba, kuna kilichorejewa awali 'umakini wa bajeti'; huwa kuna mengi ya kununuliwa wakati wa Krismasi, lakini ikumbukwe, kuna mwezi unaofuata Januari, wenye majukumu mengi zaidi.

Januari, unajulikana kuwa mwezi mgumu zaidi, majukumu ni mengi na inashauri (kama alivyoeleza Mama Waceke) ni vyema kuwapo ukomo katika bajeti binafsi.

Mwisho ambao ndio mtazamo mkuu, kuna dhana kuu Krismasi inawataka watu wafurahi; kimsingi ni wakati wa furaha. Migogoro na ugomvi sio wakati wake, hivyo ni vyema watu kuwa na amani na furaha katika siku hiyo.

***Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa mbalimbali.***

# Krismasi biashara midoli 'haishikiki'



Duka maarufu la midoli, jijini London. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

MIDOLI ina bei, tena ina biashara kubwa jijini London. Kwa mwezi Desemba peke yake mtaa maarufu wa Regent, panapouzwa midoli inatembelewa na wateja wasiopungua 650,000.

Mwenye duka mbobezi wa shughuli hiyo, Sumeet Yadav, anasema kabla ya kuuza wanafuatilia dunia nzima kujua ni aina gani wateja wao wanataka katika msimu uliopo wa Krismasi.

Hapo wenye maduka hufunga safari katika maeneo tofauti duniani, wanatembelea masoko na maonyesho kupata usahihi kinachotakiwa na wateja, kabla ya kuleta bidhaa dukani.

Yadav, mwenye asilia ya Kihindi, anafafanua undani wa biashara ilivyo kwa kauli: "Kwa kiasi fulani ni sayansi na kiasi fulani ni bahati."

Hapo anafafanua maana ya sayansi, kwamba ni ujuzi wa mchuuzi kuainisha mwenendo wa jamii na mahitaji na midoli, ili kuwaridhisha na familia wakafurahie bidhaa majumbani mwao.

Anaendelea kwamba, kuna midoli iliyotamba zamani, ndio inaanza kurudi sasa na imeongezewa teknolojia, lakini changamoto iliyopo ni kupata midoli ambayo watoto 'wanaikubali' na jambo kubwa ni watengenezaji kuwa na ubunifu wa uhakika.

Yadav anasema, hata hivyo utundu wa watengenezaji kunasa hisia za watoto unaonyesha mafanikio kuanzia mwaka jana, kwani mauzo yamepanda kupitia wachuuzi ambao ni wao.

Anasema, kuna baadhi ya wauzaji ndio wakubwa duniani wenye maduka makubwa katika takriban nchi 150 duniani kote, baadhi zikiwa na majina yaliyotukuka.

> **"Kuna baadhi ya wauzaji ndio wakubwa duniani wenye maduka makubwa katika takriban nchi 150 duniani kote, baadhi zikiwa na majina yaliyotukuka.**

# Apora pesa za benki, azigawa 'heri Krismasi'



Mtuhumiwa David Oliver. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

KRISMASI ya safari hii imekuja na yake. Jambazi wa uporaji benki kwa kutumia silaha, 'mbabu' anayesadikiwa kuwa na umri miaka 65, amekuja na kioja cha aina yake.

Aliiba ndani ya benki siku mbili kabla ya Krismasi na kisha alipotoka alitimua mbio na kurusha pesa akiwaambia 'Krismasi njema.'

Baada ya hatua hiyo, inaelezwa kwamba wapita njia na walioko jirani baada ya kuona pesa zile zinatawanywa, walikurupuka kugombania, kila mtu akiwania kuambulia walau chochote.

Polisi wa jijini Colorado, Marekani wanamtaja mtu huyo kuwa ana sura ya kizee mwenye 'madevu meupe' na tayari wamesambaza picha wanayodai kuwa yake.

"Alianza kutoa pesa kutoka katika kasha lake na anasema 'Merry Christmas' (Krismasi njema), anasimulia shuhuda anayejitanbulisha kwa jina la Dion Pascale.

Katika mbwembwe zake, inaelezwa baada ya hapo alisimama mbele ya mgahawa jirani, akisubiri kukamatwa.

Hadi sasa Polisi walishanasa jina lake mtuhumiwa, wakilitaja ni David Oliver.

UCHUMI

WANAOUNDA MATABIBU...

# Chuo Kikuu Bugando wafurahia siku yao wakipanda miti watakapohamia

## • Wanafunzi, watumishi wote 'hapa kazi tu' • Prof. Rugabaramu: Tutajenga na hospitali • Simba vs Yanga wachuana kwa bao, drafti

INATOKA UK.13

Ni sherehe iliyofanyika katika eneo la chuo lililoko Kahama -Buswelu na Kabuholo katika Wilaya ya Ilemela, Mwanza na Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Paschalis Rugarabamu, anasema jukumu kuu katika maadhimisho ya mwaka huu ni kupanda miti katika eneo hilo.

Profesa Rugabaramu, anasema chuo kimetenga kila siku ya Desemba 20 ya mwaka kwa sherehe hiyo, ikisaidia kuwawezesha wafanyakazi wake kutafakari walichokifanya katika mwaka mzima, ikiambatana na michezo na burudani.

Pia anasema sherehe zitakuwa na kawaida ya kutembelea maeneo inayoyamiliki; Kabuholo na Kahama-Buswelu jijini hapa kutathmini, chini ya ajenda ya utekelezaji malengo ya miaka 50 ijayo katika upanuzi na ujenzi wa taasisi ndani ya Mwanza.

"Chuo chetu cha CUHAS Bugando tumeweka malengo ya miaka 50 ijayo kuanza upanuzi wa ujenzi wa taasisi yake, ili kiweze kujitegemea na kupisha ndani ya jengo la Hospitali ya Kanda ya Ziwa Bugando, kwa faida ya vizazi vijavyo," anasema.

Profesa Rugarabamu, anataja malengo mengine ya sherehe ni kupanda miti kwenye maeneo hayo ili kutunza mazingira, wafanyakazi kufahamiana, chuo na Hospitali Bugando, kula na kunywa kama tumu moja inayoshirikiana kikazi.

Makamu Mkuu wa Chuo, anasema sasa ni mwaka wa tano sherehe hizo kufanyika ikiwa na faida ya kufikia vizazi vijavyo, hasa baada ya chuo kupanuliwa na jamii inayozunguka kufaidika na huduma zake, ikiwamo ajira na biashara.

Jumla ya miti 4,000 iliyopandwa kutoka lengo halisi kufikisha jumla ya miti 6,000 katika eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 200. Uhitaji halisi ni kupandwa miti 20,000.

"Kwanza malengo yetu ya awali chuo chetu tulikusudia kupata eneo la ekari 1,000, lakini tukapata hizo 200. Kutokana na maono yetu ya mbele zaidi, ndiyo maana tumeweka malengo ya miaka 50 ijayo kufanya upanuzi wa ujenzi wa chuo chetu, ili tuweze kujitegemea taasisi yetu na tutoke ndani ya eneo la Hospitali ya Kanda ya Ziwa - Bugando.

"Tunatumia kwa sasa uelewa wetu wa kuona mbele zaidi, baadaye tutaandika miradi, hivi sasa fedha zote tunazotumia ni mapato yetu ya ndani, hakuna mfadhili aliyetusaidia.

"Chuo hiki kikijenga majengo yake, tutaweza kuingia ubia na kuwekeza, pia huduma ya 'super market' (maduka ya kisasa) ili watu waweze kufanya biashara zao na kunufaika na chuo chetu anasema.

Shughuli ya upandaji miti, ulifanyika kwa kujumuisha zaidi ya wanafunzi 100 wa chuo hicho, lengo ni kujifunza stadi za maisha nje ya vitabu vya tiba na famasia wanayojifunza.



Makamu Mkuu wa Chuo cha Sayansi ya Tiba ya Afya za Binadamu Bugando (Cuhas), Profesa Paschalis Rugarabamu (wa pili kulia), akifurahia jambo na mfanyakazi wa chuo hicho, wakati wa chakula katika sherehe iliyofanyika eneo la Kahama-Buswelu Wilaya ya Ilemela, Ijumaa iliyopita.

> **"Tunatumia kwa sasa uelewa wetu wa kuona mbele zaidi, baadaye tutaandika miradi, hivi sasa fedha zote tunazotumia ni mapato yetu ya ndani, hakuna mfadhili aliyetusaidia.**



Watoto wa makazi jirani kulikofanyika sherehe, wakishiriki mlo. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS.**

### MIKAKATI ILIYOPO

Profesa Rugabaramu, anataja mikakati yao baadaye ni kuhakikisha wanafunzi wa mwaka wa nne na tano kwenye chuo hicho, wanapata mafunzo ya vitendo nje ya vitabu vya udaktari na famasia, wakiwaona wagonjwa wao.

"Upanuzi wa chuo chetu Bugando, tunapenda eneo hilo liwe la mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa mwaka wa nne na tano wanaoona wagonjwa," anasema na kuendelea: "Taasisi za utafiti zinazoshirikiana na sisi ziweze kushiriki pamoja na wafanyakazi ili kuweza kutafakari mbele zaidi."

Anataja hatua nyingine ni kuweka uelewa wao wa sasa, miongozo ya vizazi vijavyo katika malengo ya miaka 50 ijayo katika jamii inayowazunguka.

Makamu Mkuu wa Chuo Bugando, anasema eneo pia linahitaji katika mipango ya baadaye, kujengewa maeneo ya kutembea kwa miguu, kukimbia na kupumzika.

Profesa Rugabaramu, anaendelea ufafanuzi wake kwamba barabara zilizopandwa miti siku hiyo, akizitaja 'nne za msalaba' na 'mbili za mzunguko' miti ya mbao na vivuli na kuongeza miti iliyopandwa awali na kukauka itapandwa tena.

### KAMATI STAREHE

Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa na Starehe, ambaye ni Mhadhiri katika Idara ya Maabara, pia Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Cuhas, Mujungu Geofrey, katika wasilisho lao wanasema bajeti ya sherehe ni Sh. milioni 10.

"Tumewashirikisha wafanyakazi wa Hospitali ya Kanda ya Ziwa -Bugando na wanafunzi 120 wa chuo. Lengo ni kutafakari tulichokifanya mwaka mzima, kushiriki pamoja kabla ya sikukuu za Krismasi za kufunga mwaka na watu kwenda kupumzika makwao.

"Ndiyo maana unaona sherehe zetu zinakwenda sambamba na za wafanyakazi wa Hospitali ya Kanda ya Ziwa- Bugando kila mwaka, ambazo tunaziita Cuhas Bugando Day, kwa sababu tunafanya kazi pamoja, ikiwamo kula na kunywa pamoja, kufanya michezo na burudani ili kuondoa msongo wa mawazo kwa wafanyakazi," anasema Geofrey.

Kiongozi huyo wa kamati anasema, malengo ya kila mtu ilikuwa kupanda miti 40 na kuchangia 'harambee' ili kuitunza, pia kuongeza matawi mengine ya chuo kiweze kupanuka zaidi katika utoaji wa huduma zake.

Kila mfanyakazi katika sherehe kupitia 'harambee' alichanga fedha Sh. 50,000, kwa ajili ya kutunza mti kwa mwaka mzima, kuumwagilia maji.

Noris Frank, ni Ofisa Utumishi Mwandamizi wa Cuhas Bugando, anayeeleza kufanyika sherehe za namna hiyo, zinasaidia kuboresha ufanisi na mipango mipya ya baadaye.

"Upanuzi wa chuo chetu kwenda eneo la Kahama-Buswelu ni moja ya tija kubwa katika kuboresha elimu na kuondoa uhaba wa wafanyakazi wa idara ya afya (kitaifa). Pia majengo yake yatasaidia kuwepo vitega uchumi zikiwamo kumbi za mikutano," anasema Frank.

Anasema matarajio yao ya baadaye ni kutaka chuo kikue zaidi hamasa mojawapo ikipitia uboreshaji wa maendeleo ya chuo hicho.

### MICHEZO YAFANA

Ni halfa iliyonogeshwa na michezo mbalimbali kwa wafanyakazi wa jinsia zote; wanaume na wanawake, kukishuhudiwa bao, kuvuta kamba na kucheza drafti, kupitia upinzani wa utani wa vilabu vya Simba na Yanga.

Michezo mingine ni pamoja na kushindana kujaza maji kwenye chupa za soda, kugani mashairi, danadana za mpira wa miguu wanaume na kucheza muziki. Ni ushindani ulioishia wapenzi wa Yanga kushinda michezo minne dhidi ya mitatu kwa Simba.

Hayo ni mambo yaliyoambatana na kuburudika kwa vinywaji mbalimbali, iliyoambatana na ushindani wa kusakata muziki kati ya wafanyakazi na wakazi wa jirani walipishana na nguvu na kutoka sare katika mchuano huo uliofurahisha.

Aidha, katika tukio hilo, watoto nao walishiriki chakula na kusakata muziki, huku mlipuko wa burudani ukitawala.

***Mwandishi anapatikana kwa barua pepe: anthonygervas@yahoo.com na simu: (+225) 0682 86 92 44 Kanda ya Ziwa.***



Wafanyakazi wa Chuo cha Sayansi ya Tiba za Afya ya Binadamu Bugando (Cuhas) na wanafunzi wao, wakicheza bao kwenye eneo la chuo hicho.

# Biashara katika picha



Baadhi ya wanachama wa vikundi 20 vya wakulima wa Musoma Vijijini mkoani Mara, wakiwa na majembe ya kukokotwa na ng'ombe ambayo ni miongoni mwa 20 waliyopewa juzi na Mbunge Prof. Sospeter Muhongo, ikiwa ni mwanzo wa kampeni ya kuacha kilimo cha jembe la mkono. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**



Biashara ndogo imekuwa ni mkombozi kwa baadhi ya watu sehemu mbalimbali nchini. Pichani wateja wakinunua bidhaa kwa Machinga eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana.



Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Msingi Umoja cha Mjini Liwale mkoani Lindi, Hassan Mpako, ambaye ni mhamasishaji wa kilimo cha alizeti wilayani Liwale, akiwa kwenye shamba lake la zao hilo hivi karibuni.

UCHUMI

# Simulizi inayodondosha chozi atoayo binti maskini wa kutisha

• 'Ng'ombe wa maskini hazai' ilivyotimu • Sasa athibitisha 'mvumilivu hula mbivu'



Jane Kiarie akitoa misaada kwa wanafunzi wenye shida kupitia mradi wake. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Maalum**

JANE Kiarie, ambaye mama yake alinuia mimba yake kuitoa 'ikagoma' alizaliwa akiwa na miezi minane na mama yake akamtelekeza.

Mama huyo alipata mimba na kijana mwenye umri wa miaka 17 wakati huo akiwa mwajiriwa wa kazi za nyumbani, jijini Nairobi.

Namna alivyoachwa ni baada ya mama kuiona mzigo na haimudu tena, alimwacha mtoto kwa dada yake (mama mkubwa wa Jane), alikokuwa anaishi.

Simulizi zinasema mama huyo baada ya kuona tendo la kutaka kutoa mimba ya miezi minane, linaangukia mtoto kutoka na analia, akaamua kumuacha mtoto na kutoweka.

Dada yake aliporudi jioni baada ya pilika za siku, akakutana na maajabu ya mtoto nyumbani kwake akiwa peke yake. Alichoamua kufanya ni kumpeleka kwa bibi yake. Yote ni mtihani wenye mzizi wa ugumu wa maisha.

Masahibu ya mzazi huyo hayakuishia hapo, kwa sababu alirejea tena miaka minne baadaye, wakati huo Jane akiwa na umri wa miaka 21 na ana mtoto mwingine wa kike mgongoni.

Safari hiyo, Jane anasimulia kwamba mama huyo alionekana kuwa na mpango madhubuti kwa watoto wake. Kila mara safari hiyo aliwatembelea na kuwaletea viatu, pesa za matumizi na maisha yakaendelea.

Lakini ni penzi lililodumu kwa miaka miwili tu. Jane anasumulia: "'Namshukuru mama yangu, kwa sababu aliamua kubeba ujauzito wangu, badala ya kuitoa nikiwa na miezi kidogo tumboni mwake."

> **"Nilichofanya ni kwenda kwa mkuu wetu wa shule na kumwomba nilime shamba lake kwa Jumamosi nne kuanzia asubuhi mpaka jioni na yeye anilipie mtihani.**

Baada ya mama huyo kutoweka kwa kipindi kifupi, bibi yake Jane alipata taarifa kuwa mtoto wake (Mama Jane) amefungwa jela.

"Wakati huo mama yangu alikuwa akifanya biashara yake katika soko la Gikomba Viungani mwa Nairobi na siku moja watu wakaiba viatu katika duka moja la Mhindi usiku. Watu walioiba viatu hivyo wakamuuzia mama," anasema.

Jane anasimulia msako ulivyofanywa na viatu vyenye namba sawia na vilivyoibwa vikapatikana kwake. Mama huyo akafungwa na alipotoka, Jane alikuwa amefikika darasa la nne na bibi yake hakuweza kumudu karo ya shule na akalazimika kumwachisha mjukuu shule.

"Mama aliachiliwa huru baada ya kuhudumia kifungo chake, lakini akarejea akiwa mtu tofauti," anasimulia Jane, akisema mama huyo alikuwa anaumwa kifua kikuu na hakukuwapo na dawa za kumhudumia kutokana na uwezo duni.

Jane anasema, baada ya kumwona mama yake akiteseka, aliamua kujitosa katika ajira kama aliyotumikia mama yake, akiwa na umri wa miaka 10, akipigana kukabili umaskini wa nyumbani.

"Sikuwa naweza kupika, lakini jukumu langu lilikuwa kumwangalia mtoto na kumlisha na kuosha nguo," anasimulia Jane na anaongeza: "Nilikuwa nikilipwa shilingi elfu moja ya Kenya na wakati huo ilinisaidia pakubwa."

Katika kipindi cha miaka miwili, mshahara wake ulienda moja kwa moja kwa bibi yake, ili mama yake apate matibabu.

"Woga wangu ulikuwa ni kwamba mama hataweza kurejea katika hali yake ya kawaida," anasimulia kwamba katika kipindi mama yake yu hoi kitandani, ndoto aliyokuwa akiisimulia bibi yao ni moja tu, kuona watoto wake wanarudi shuleni.

Lakini kwa bahati mbaya, mama huyo aliaga dunia muda mfupi baadaye.

### BAADA KIFO

"Haikuwa kazi rahisi, kwa sababu kwanza sikuwa nimejaliwa kuishi naye na miezi mitano tu baada ya yeye kurejea na kuanza kujenga uhusiano wa mama na mtoto, akaaga dunia," anasema.

Jane anadokeza hakumjua baba yake na bibi yake anatoka jamii inayoamini katika kutimiza wosia wa mtu aliyekufa, hivyo alifanya juu chini kuhakikisha wajukuu wake wanarejea shuleni.

Mjukuu Jane anasema, baadaye alijiunga na darasa la tano, huku dada yake akiingia darasa la tatu. Hata hivyo, changamoto za maisha ziliendelea kuongezeka kila kukicha na hawakuwa na uwezo wa kujikimu mahitaji yao.

Hapo anaorodhesha karo na mahitaji ya shule, huku wakikutana na shule na watoto wa familia ambako binafsi alikuwa akifanyia kazi.

"Nikiwa darasa la nane kuna pesa zilizokuwa zinahitajika, Sh. 550 kwa ajili ya mtihani wa mwisho wa darasa la nane na sikuwa na mtu wa kunilipia.

"Nilichofanya ni kwenda kwa mkuu wetu wa shule na kumwomba nilime shamba lake kwa Jumamosi nne kuanzia asubuhi mpaka jioni na yeye anilipie mtihani," anasimulia Jane.

Anasema japo alifaulu mtihani wake, alikosa mtu wa kumwendeleza akaamua kurejea kufanya kazi za nyumbani.

### MWANZO MABADILIKO

Jane anasema, baadaye aliishi kwa shangazi yake aliyeamua kumpeleka katika shule ya kutengeneza nywele na akapata kazi kwenye saluni, japo mshahara ulikuwa mdogo sana.

Anasema, kasisi wa kanisa ambalo alikuwa anaabudu, alifahamu simulizi yake na kwamba wao ni yatima, akaanza kuelekeza huruma yake huko.

"Dadangu (mdogo wake) hakumaliza darasa la nane kwa sababu ya ukosefu wa karo," anasimulia, kwamba kasisi wao aliamua kumchukua Jane kama mtoto wa familia yake ndio ukawa mwanzo wa maisha yake kufunguka.

Familia hiyo ilimtafutia usaidizi kwa wahisani na hatimaye Jane alifanikiwa kurejea shuleni, mnamo Februari mwaka 2001 wakati alipojiunga kidato cha kwanza katika Shule ya Juja.

Safari yake haikuwa rahisi, kwa sababu ya malimbikizi ya madeni, lakini utawala wa shule ukamruhusu kufanya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2004.

### NGAZI ZAIDI

Mwaka huo baadaye, Jane alikutana na Wamishionari wawili waliokuja kanisani mwao na baada ya kufurahishwa na muziki wake, walimpa fedha shilingi 42,000 za Kenya (Sh. 956,256) akajiunga na shule ya muziki na pesa zilizosalia, wakazitumia kumalizia ada ya shule aliyokuwa anadaiwa.

Jane aliolewa mwaka 2008 akiwa mtu wa pili katika familia yake kufanya harusi na kila mtu alitaka kujua kama ni ukweli anaolewa.

Akapata mtoto wa kwanza mwaka 2011, lakini kwa bahati mbaya miezi 10 baadaye alipata homa kwa siku mbili na akafariki.

Jane anasema alipata ujauzito tena lakini ikatoka, ikiwa na miezi miwili. Baadaye alijaliwa kupata mtoto wa kike mwenye umri wa miaka sita sasa.

Anasema, hivi sasa ameegemea sana imani yake kidini, kama msingi wa maisha yake.

Pia amefungua mradi wake wa kufundisha watoto wasiojiweza na kwa sasa amefanikiwa kusomesha watoto watatu wa kike kama njia moja ya kurejesha shukrani kwa jamii. **BBC**

UCHUMI

# Darasa linalovutia kutoka staili ya mkakati maendeleo bara Asia

**Na Nimi Mweta**

UKIPITA mitaa ya Jiji la Dar es Salaam ukaona viwango vya utengenezaji wa barabara, mitaro na kufunga taa, unaanza kujiuliza fedha hizi zimetoka wapi, wakati zamani ilikuwa ni jambo ambalo halifikiriki, ila kwa barabara kubwa chache baadhi wakibeza 'yanakopita magari makubwa'.

Hivi sasa wengi zaidi wamehama. Kilele cha mabadiliko hayo ni Wizara ya Fedha na Mipango (Hazina) kukiruhusu Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kutumia majengo ya mtaa wa Madaraka kama madarasa. Ilikuwa ndiyo maskani nyeti ya kuamua mambo muhimu ya uendeshaji uchumi nchini.

**KUTOKA ASIA**

Somo la msingi kutoka nchi za Asia, ambalo pia walilichukua Ulaya lilikotumika kwa miongo kadhaa karne iliyopita, ilikuwa kupunguza mijadala katika masuala ya uchumi na sera, ili kuweka mkazo katika utendaji, na kujenga mshikamano unaohitajiwa.

Moja ya maeneo ambayo yamelalamikiwa sana tangu Afrika ipate uhuru ni 'eating chiefs' kwa maneno ya mtunga riwaya wa Cameroon, Elechi Amadi, yaani machifu walaji, ambayo haina maana ya ulafi ila upigaji dili.

Mwalimu Julius Nyerere, alijaribu kupambana na hali hiyo alivyoweza, lakini ilikuwa imeota mizizi, kipindi cha demokrasia ya vyama vingi kikakoleza matatizo, kwani aliyeko madarakani anahitaji marafiki, kampeni.


Mtaalamu wa uchumi mwenye nishani ya Nobel na zamani Mchumi Mkuu wa Benki ya Dunia, Profesa Joseph Stiglitz, alisisitiza umuhimu wa upatikanaji kodi kiasi kinachopasa na kuitumia inavyostahili kwa maendeleo.

Ilikuwa ni semina ya kimataifa jijini Dar es Salaam, kuwasaidia watunga sera kupambanua masuala kadhaa ya kisera, kwa mfano uhusiano kati ya mipango ya maendeleo na mazingira wezeshi ya kufanya biashara, kipi kinatangulia na kwa vipi.

Siyo rahisi kusema kama kulikuwa na 'muafaka,' lakini umuhimu wa kodi na miundombinu kama sehemu ya mazingira wezeshi kibiashara na siyo misamaha ya kodi irundikane ni somo ambalo limesisitizwa miaka kadhaa.

Ukizungumzia katika mustakabali wa mlinganisho wa mifumoo ya siasa na uchumi duniani, kuna walakini kuwa zipo tofauti katika kina cha kuvunja mifumo ya jadi kijamii kuwa ya kisasa, kwani ni kuporomoka mifumo ya jadi kunakowezesha iwepo mifumo shindanishi.

Ndiyo msingi wa uchumi wa soko na inafaulu kujenga nidhamu kwanza katika soko, halafu katika utawala, kupitia ushindani halisi.



Rais John Magufuli, akiangalia moja ya hatua za mwisho katika utengenezaji wa mifuko ya sandarusi katika kiwanda kilichoko Shinyanga.
**PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **"Mtaalamu wa uchumi mwenye nishani ya Nobel na zamani Mchumi Mkuu wa Benki ya Dunia, Profesa Joseph Stiglitz, alisisitiza umuhimu wa upatikanaji kodi kiasi kinachopasa na kuitumia inavyostahili kwa maendeleo.**



Kiwanda kipya nchini kikiendelea na uzalishaji.

Huo ni mifumo ambao kila mtu anaishi kwa kujali ndugu na jamaa zake wanamwangalia kivipi, kama ana gari au hapana, ana nyumba wapi, ikoje...

Katika mazingira hayo, kuna kichocheo kikubwa cha rushwa kwa maana ya kuvuruga mipango ya ununuzi iendane na maslahi ya wanaofanikisha zoezi hilo na siyo kampuni wanazowakilisha au idara za serikali.

Pale ambako kampuni binafsi inafanya ununuzi kutoka kampuni nyingine, viwango vya rushwa vinakuwa vidogo kwani kila utawala wa kampuni unahisia kali kiasi kuhusu bei na matumizi, tofauti na ununuzi wa umma.

Hapo hakuna anayepata hasara, labda walio juu wahoji kilichotokea na endapo taratibu za kupeana taarifa zinafuatwa, huenda suala hilo hata lisifike mezani. Ni mojawapo ya maeneo ambayo somo la Asia lilirekebisha, kuwapunguzia uhuru.

Hivyo watawala wakijua kuwa ununuzi au ujenzi fulani utafuatiliwa kwa kina hawatakuwa na nafasi ya kufanya manunuzi potofu iwe ni kwa viwango vya bidhaa au bei, na kwa maana hiyo mfumo wa ufuatiliaji inabidi uweke kando uhuru wa uamuzi na taratibu za kupeana habari bila kuzikagua.

Inafika hatua wananchi wanakuwa na ujasiri wa kutaka kueleza kero na jinsi zinavyochangiwa na hujuma za viongozi kukusanya vipesa kwa miradi yao binafsi ndipo hali hiyo irekebishwe, mazingira ambayo kwanza yanahitaji kuondolewa uhuru wa kufanya uamuzi kwa ngazi za kirasimu bila kuhojiana.

Ni somo mojawapo la Asia la kusimamia utekelezaji bila kuzuiwa kirasimu. Yako maeneo ya Asia ambayo bado hayajafanyiwa kazi, lakini mikutano inayoendelea kati ya makundi au chemba za biashara na hata vyama vya kijamii kuunganisha nguvu katika maeneo fulani huenda ikazaa matunda.

Mojawapo ni kujenga mwingiliano wa uwezo wa kiufundi, raslimali na uendeshaji, kwa kuchangia hisa katika kampuni, ambako raslimali kianzio inakuwa na thamani kiasi fulani ya hisa, kwa mfano asilimia 70 kwa kuzingatia ardhi na majengo, vifaa tangulizi.

Halafu kampuni ya nje inaingiza mitambo mipya na kuhakikisha upenyezaji wa teknolojia hiyo kwa wafanyakazi au wataalamu wazawa, ili iwe endelevu katika njia tofauti na kununua leseni yao.

Kumekuwa na msukumo mkubwa miaka ya karibuni kurudisha umiliki moja kwa moja katika kampuni kadhaa, nchini, lakini kuna hali ya kusuasua kiuwekezaji, kama viwanda vya nguo vya zamani.

Mkakati wa sasa wa kuweka mazingira wezeshi kibiashara inabidi upige hatua nyingine katika kutumia mifumo ya Asia, ambako wageni wamekuwa wakinunua hisa za kampuni na kuinua 'brand' bora.

UCHUMI

# Neema ya uchumi wa kisasa kwa wanaokimbia shida kuu ukeketaji

• Shule ya kilimo, ufugaji, ujasiriamali • Wakihitimu 'baibai' maisha utegemezi



Ngoma ya asili ya 'litungu' ikitumika kuhamasisha jamii kuachana na ukatili wilayani Serengeti, huku mabinti na Mkurugenzi wa Shirika la Hope, Rhobi Samwelly (nyuma ya wasanii) wakicheza. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

MATATIZO yanayowakumba wasichana ni mengi, ikiwamo ubaguzi, ukatili wa kijinsia kama kukeketwa, kudhulumiwa haki zao za kupata elimu, ndoa za utotoni, ambavyo kwa ujumla wake vinakatisha ndoto zake.

Kwa ujumla, wasichana ni waathirika wakubwa wa majanga hayo, ambayo kila kukicha yanakemewa na serikali na wadau mbalimbali wanaopiga vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii.

Pamoja na marufuku ya serikali, bado vipo kwenye baadhi ya maeneo nchini na vinafanyika kimya kimya, lakini wadau wa kupinga ukatili wanawagundua kufikisha taarifa kwenye vyombo vya dola.

Hope for Girls and Women Tanzania, ni miongoni mwa wadau hao, wanaojishughulisha na vita dhidi ya vitendo vya ukeketaji wa mabinti, wilayani Serengeti mkoani Mara, ikiwa na maskani yake mjini Mugumu.

Katika eneo hilo kuna 'nyumba salama' mbili za Mugumu na Butiama, inayotoa elimu kuhusu madhara ya ukeketaji na kuibua siri za vitendo hivyo wilayani humo.

### DARASA KILIMO, UFUGAJI

Wakati likiendelea na kazi hiyo, sasa linajipanga kuwafundisha mabinti waliokimbia ukeketaji na kulelewa na nyumba salama za shirika hilo, kilimo hai na ufugaji wa kisasa, ili baadaye wawe wakulima bora na wajasiriamali.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Rhobi Samwelly, anasema njia hiyo itawasaidia kujitegemea kiuchumi kwa kutumia elimu wanayopata katika nyumba salama za shirika hilo, badala ya kuachwa wakihangaika mitaani.

Rhobi anasema, tayari wameshapata eneo la ekari 20 zilizopo nje ya 'Mji wa Mungu' zitakazokuwa makao makuu mapya ya shirika, huku kukiwapo shughuli za ujasiriamali na mafunzo ya kilimo hai na ufugaji wa kisasa.

> **"Hayo yote hatuwezi kuyafanya katika eneo la sasa ni dogo ambalo hata majengo yake ni madogo, hayatoshi kuweka vitanda vya ziada, hivyo hatuna budi kuhamia kwingine.**



Mkurugenzi wa Shirika la Hope, Rhobi Samwelly, akielezea mikakati ya kuanzisha mafunzo ya kilimo hai na ufugaji wa kisasa kwa mabinti wanaolelewa na nyumba salama za shirika hilo.

Mkurugenzi huyo ameiambia Nipashe kuwa mmoja wa wafadhili wa Hope for Girls and Women Tanzania, anayemtaja kwa jina la Singita Grunet, amenunua ekari hizo ili asasi ipanue shughuli zake.

"Hope ina wafadhili mbalimbali wakiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA), Ubalozi wa Canada, Four Seasons Serengeti na hao Singita Grunet, waliotununulia eneo, lakini pia Canada wametusaidia Sh. milioni 72 za kuanzia," anasema.

Anasema, shirika linaendelea kusaka msaada kwa wafadhili, ili kutimiza lengo kupanua shughuli zake kwa kujenga nyumba salama mpya kwenye eneo lao ambamo kutakuwa na shughuli mbalimbali za ujasiriamali.

### ENEO JIPYA

Katika upanuzi huo, anasema Taasisi ya Hope inatarajia kuanzisha ufugaji, kilimo hai, ufugaji wa kisasa wa kuku na ng'ombe, madarasa ya ufundi wa aina mbalimbali, lengo kuu likiwa ni kuwapatia mabinti ujuzi wa uzalishaji mali na kujiletea maendeleo mara wanapoamua kurudi nyumbani kwao.

"Kilimo ni msingi wa maisha ya binadamu na kwa Mtanzania, kilimo ni uti wa mgongo wa taifa, kikiwa kinachangia asilimia kubwa ya pato la taifa, na pia kilimo ni mwajiri wa takriban asilimia 80 ya Watanzania," anasema.

Rhobi anasema, kwa sasa kilimo hai na ufugaji wa kisasa ndivyo vinavyohimizwa, huku kilimo hai kikitumia mbolea isiyotengenezwa viwandani, na kwamba kinazingatia utunzaji wa mazingira.

"Kimsingi ni kwamba eneo ambalo nyumba salama ya Mugumu ipo ni dogo, hali inayosababisha kuwa na mabweni yenye upana mdogo ikilinganishwa na idadi ya mabinti 67 waliopo," anasema.

Anasema, madarasa pia ni machache, hali inayolazimu masomo yote kufundishwa sehemu moja na kuwanyima wanafunzi wa ufundi sehemu ya karakana kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

Anasema, kwa kuwa wameamua kujikita kwenye ujasiriamali kwa lengo la kuwasaidia mabinti kupata ujuzi na utaalamu wa mambo mbalimbali ya biashara, eneo lao la ekari 20 linaweza kutosha kwa yote hayo.

Mkurugenzi huyo anasema, Hope inataka kuona mabinti wanaofika nyumba salama, wanarudi kwao na kuanzisha biashara au kilimo cha mazao ya biashara ambacho kitawapa faida kwa vile tayari watakuwa na ujuzi.

### HIVI SASA?

Rhobi anasema, kwa sasa mabinti hao wamekuwa wakijifunza ufundi wa kushona, ujasiriamali, sheria, Kiingereza, hisabati, masomo ya kawaida ya kimtaala, kuhusu madhara ya ukeketaji na afya ya uzazi.

Anasema, ipo haja sasa ya kupanua ujasiriamali kwa kuwafundisha kilimo hai, ufugaji ng'ombe na mengine muhimu ya kuwawezesha kujitegemea.

"Hayo yote hatuwezi kuyafanya katika eneo la sasa ni dogo ambalo hata majengo yake ni madogo, hayatoshi kuweka vitanda vya ziada, hivyo hatuna budi kuhamia kwingine," anasema.

Analitetea eneo jipya kwamba, linatosha kuwa na shughuli zote wanazotaka kuzifanya kwa ajili ya mabinti hao, hiyo anaomba wafadhili zaidi wajitokeze kuunga mkono mipango ya asasi hiyo.

Rhobi anaainisha wigo wa kitaaluma, kwamba mambo ya kupata uelewa sahihi wa fani ya ufundi, ujasiriamali, sheria, lugha ya Kiingereza, hisabati na kimtaala mingineyo, ikiendana na madhara ya ukeketaji na afya ya uzazi, wakiwa katika eneo la kutosha, ni mambo yatakayoweza kufanyika kwa ufanisi zaidi.

"Vitendo vya ukatili wa kijinsia ni vingi na mabinti wanafundishwa athari zake na kupewa ushauri wa kisaikolojia kutoka kwa maofisa ustawi wa jamii, kwani wapo katika nyumba zetu salama," anasema.

Anasema, kwa kuwa vitendo vya ukatili huo bado ni vingi, ana uhakika Hope itaendelea kupokea mabinti wengine wapya, hivyo ni muhimu kupanua shughuli za shirika, ili kukidhi mahitaji yao.





Wananchi wa Mtaa wa Pambogo jijini Mbeya, wakiwa katika eneo la mashamba wanayogombania na Halmashauri ya Jiji la Mbeya.
**PICHA: NEBART MSOKWA**

# Neema ruzuku yaja kwa wenye mifugo

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema imeanza kutoa ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo ili kuwarahisishia wafugaji kupata dawa hizo kwa bei nafuu kwa lengo la kuboresha mazao yatokanayo na mifugo na kuongeza tija katika sekta hiyo.

Aidha, wizara hiyo imeanza utaratibu wa kuwahamasisha wafugaji nchini kote kuwa na utaratibu wa kuogesha mifugo yao ili kukabiliana na magonjwa pamoja na wadudu wanaoshambulia mifugo na kupunguza ubora.

Hayo yalisemwa juzi wilayani Mbarali na Ofisa Takwimu wa Wizara hiyo, Makunga Seleman, wakati wa kuhamasisha wananchi kuogesha mifugo yao iliyofanyika katika Kata ya Igulusi.

Alisema serikali imeamua kuanza kutoa ruzuku hiyo kutokana na umuhimu wa sekta ya ufugaji katika kuliingizia taifa fedha nyingi kutokana na kuuza mazao ya mifugo zikiwamo ngozi pamoja na maziwa na hivyo fedha hizo kuingizwa kwenye miradi ya maendeleo.

Makunga aliwataka wafugaji kuchangamkia fursa hiyo, ili kuboresha mifugo yao na kwamba wakiiboresha hata soko litakuwa zuri na watapata tija zaidi tofauti na sasa ambapo wanafuga kienyeji.

"Lengo la Wizara ni kuhakikisha asilimia 70 ya mifugo yote nchini inaogeshwa ili kukabiliana na magonjwa ambayo yanaidhoofisha, ukipita baadhi ya maeneo unakuta mifugo ina afya za ovyo sana, sasa ukichukua mfugo kama huo ukapeleka sokoni soko lake haliwezi kuwa zuri," alisema Makunga.

Alisema hamasa hiyo kwa sasa inailenga zaidi mifugo kama ng'ombe, mbuzi na kondoo na kwamba hata wanyama kazi kama punda nao wanahusika kwenye hamasa hiyo.

Nao baadhi ya wafugaji waliishukuru serikali kwa kuanzisha utaratibu huo kwa maelezo kuwa ni mzuri na tayari wameshaanza kuyaona matunda yake kwa bei ya dawa kupungua kuliko ilivyokuwa awali.

Mwenyekiti wa kamati ya Josho la Mifugo la Kata ya Igurusi, Pius Mwandenga, alisema ruzuku hiyo ya dawa za kuogesha mifugo imekuwa na faida kubwa kwa wafugaji ikiwamo kuwapunguzia gharama za kuogesha mifugo yao.

Alisema kwa sasa kutokana na gharama kupungua hata wale wafugaji ambao walikuwa wanaogopa kuogesha kwa sababu ya kuogopa bei watahamasika na kuanza kuogesha.

Alisema kwa sasa bei ya kuogesha mifugo imepungua kwa zaidi ya nusu ya bei ya awali kwa maelezo kuwa awali ilikuwa ng'ombe mmoja alikuwa anaogeshwa kwa Sh. 200 na kila ng'ombe alikuwa anatakiwa kuogeshwa kwa miezi sita, lakini kwa sasa mfugaji anatakiwa kuchangia Sh. 600 kwa miezi sita sawa na Sh. 100 kwa mwezi.

"Sasa hii ni fursa kubwa kwetu wafugaji maana sasa tutazalisha mifugo yenye ubora kuliko ilivyokuwa awali, kuna baadhi walikuwa hawaleti mifugo kwa kuogopa gharama, lakini sasa tunawashawishi na tutatoa elimu ili waanze kuileta," alisema Mwandenga.

Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Agostino Lawi, alisema ruzuku ya dawa za mifugo inayotolewa na serikali imeongeza idadi ya mifugo inayoogeshwa kila wiki wilayani humo.

Alisema wananchi wengi wamehamasika kuanza kupeleka mifugo yao kwenye majosho na hata kiwango cha makusanyo kimeongezeka tofauti na ilivyokuwa mwanzo.

Naye daktari wa mifugo Mkoa wa Mbeya, Dickson Nyanda, alisema mkoa huo una majosho zaidi ya 80, lakini yanayofanya kazi yapo 65 na kwamba sasa mifugo itaboreka.

## Wanakijiji wajitolea ujenzi wa barabara

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANANCHI wa Kijiji cha Mapunga Kata Igurusi Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wameanza kuchimba barabara yenye urefu wa kilomita tatu kutoka katika Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam) kuelekea mashambani kwa kutumia jembe la mkono.

Wakizungumza juzi wakati wakichimba barabara hiyo, wananchi hao walisema wameamua kuanza kuchimba barabara hiyo kutokana na barabara hiyo kuwa muhimu, lakini serikali imekuwa ikiwaahidi kuiboresha bila mafanikio.

Mmoja wa wananchi hao, Joseph Moshi alisema barabara hiyo walianza kuiomba tangu mwaka 2005, lakini mpaka sasa wanaahidiwa kuwa watachimbiwa na serikali bila mafanikio.

"Wananchi tumeamua baada ya kuona serikali haionyeshi kukamilisha kipande hiki na ni barabara muhimu sana maana inatumika kuunganisha kijiji chetu na mashamba ya mpunga ambayo tunayategemea," alisema Moshi.

Alisema watoto wote wa eneo hilo wanaitumia barabara hiyo wanapokwenda shuleni na kwamba kipindi cha mvua barabara hiyo huwa haipitiki kabisa na hivyo wanaiomba serikali kuwasaidia.

Nao baadhi ya wanawake wa kijiji hicho walisema barabara hiyo ni muhimu kutokana na kwamba ndiyo wanayoitumia wanapoelekea hospitali kupata huduma za afya hasa wanapokuwa wajawazito.

Mmoja wa wanawake hao, Rehema Nyangala, alisema barabara hiyo hata pikipiki haziingii kutokana na ubovu na hivyo wamehamasika kuanza kuichimba wenyewe.

# Watafiti, watakwimu wapewa somo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATAFITI na watakwimu nchini wametakiwa kutenga muda wao wa kukutana na wananchi wa chini ili kupata majibu ya ziada katika utafiti wao.

Rai hiyo ilitolewa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alipokuwa anazungumza na wananchi wa Kata ya Forest jijini Mbeya, wakati akifanya utafiti wa hali na upatikanaji wa nishati ya umeme Tanzania Bara kwa kupata maoni toka kwa wananchi.

Dk. Chuwa alisema wananchi wanafahamu maana ya takwimu, hivyo ni muhimu kwa watafiti na watakwimu wote nchini kuhakikisha wanakutana na wananchi wa kawaida vijijini na mijini ili kupata maoni na majibu ya ziada kwa lengo la kupata majibu ya 'kwanini'.

"Wadadisi wote watumie muda wao na wasimamizi na watakwimu wote wa mikoa yote nchini wafanye kazi ya kukutana na wananchi, waweze kupata majibu ya ziada ya kuongezea kwenye uchambuzi wa utafiti utakaofanyika.

Alisema katika mikutano yake ya kukutana na wananchi kupata maoni tofauti nchini, amebaini wanaelewa umuhimu wa takwimu na kazi yake.

Alisema kutoa taarifa za takwimu ni suala shirikishi na ni suala la kikatiba kwamba serikali ipate taarifa na mwananchi atoe taarifa iliyosahihi, ili mwisho wa siku mwananchi aibane serikali kwamba alitoa taarifa ya jambo fulani je, aliifanyia kazi?

Alisema serikali itaendelea kutoa ushirikiano wa dhati kwa wananchi katika utafiti wa takwimu wanazozifanya ili kuona mambo yote yanayojitokeza yanashughulikiwa ipasavyo kwa kuwa wana takwimu halisi za jambo husika.

Awali wananchi hao walimweleza Dk. Chuwa na timu yake kwamba hali ya upatikanaji wa nishati ya umeme kwa maana ya kupata mwanga kwenye nyumba zao ipo vizuri na umefika maeneo mengi ya vijijini na mijini, lakini tatizo wanalokumbana nalo hivi sasa ni gharama zake kuwa juu.

Mkazi wa Mtaa wa Muungano, Kata ya Forest jijini Mbeya, Solomon Mwandenuka, alisema umeme kwa ajili ya mwanga nyumbani kwao sio shida kubwa kwa sasa, lakini kinachowaumiza ni gharama kubwa jambo linalowafanya kushindwa kumudu.

"Tunachohitaji hivi sasa tupate umeme kwa gharama nafuu zaidi ili tuweze kuanza kupikia chakula badala ya kuendelea kutumia kuni, na hili kuni ndilo linafanya wake zetu kuzeeka mapema kutokana na moshi wanaokumbana nao," alisema Mwandenuke.

Aliiomba serikali ishushe gharama za nishati hiyo ili wananchi waachane kabisa na matumizi ya kuni na mkaa kupikia vyakula na hivyo kupunguza hata ukataji miti kwa ajili ya nishati.

Naye Mzee Rhone Chilewa, mkazi wa Forest, alisema kutokana na kupatikana kwa nishati ya umeme maeneo mengi, vijana wengi hivi sasa wamejiajiri wenyewe kwa kufungua viwanda kama vile vya kupasua mbao, kuchomelea vyuma na maeneo mengi hususani vijijini karibu kila nyumba ina umeme.





# Askofu ataka tume huru ya uchaguzi

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

ASKOFU mstaafu wa Kanisa la Baptist Jimbo la Dodoma, Anthony Mlyashimba, ametaka kuundwa kwa tume huru ya uchaguzi.

Aidha, askofu huyo amewata viongozi wa dini nchini kukemea vitendo vya watu kupotea katika mazingira ya kutatanisha.

Askofu huyo mstaafu alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ibada ya kumbukizi ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo katika kanisa hilo, lililopo Mombasa Makole jijini Dodoma.

Askofu Mlyashimba alisema kuwa kuna haja ya kuwapo kwa tume huru na haki ya uchaguzi ili kuondokana na malalamiko.

Alisema mfano mzuri ambao unaonesha umuhimu wa kuwa na tume huru na haki ya uchaguzi ni kutokana na malalamiko na malumbano yaliyojitokeza wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa.

"Tukumbuke kauli mbiu ya Rais wa awamu ya tatu Benjamini Mkapa ya ukweli na uwazi, kauli hiyo ndiyo inayoweza kuondoa utata na malalamiko ya wanasiasa.

"Itakuwa ni ajabu kama itaundwa tume huru na haki ya uchaguzi na kusikia mwanasiasa analalamika kuwa ameonewa kwani mtu huyo ataonekana kama punguani kutokana na kila kitu kuwa wazi.

"Kinachoweza kutokea ni nini kama Watanzania kukosa wanachokihitaji?" Alihoji na kuongeza:

"Ni kujikuta wanafanya maamuzi ambayo si sahihi wakati mwingine kusababisha machafuko."

Pia alisema kuna haja kubwa ya msimamizi wa tume ya uchaguzi na msajili wa vyama vya siasa kuwa na hofu ya Mungu pamoja na kuwa na macho ya kiroho katika kufanya maamuzi.

Alisema kama viongozi hao hawatakuwa na macho ya kiroho na kuona kuwa wanafanya kazi kwa ajili ya kuwafurahisha wakubwa wao bila kumwogopa Mungu wataliweka taifa pabaya.

Akizungumzia matukio kadhaa ya kupotea kwa baadhi ya watu, alisema suala hilo linatia aibu kwa taifa.

Alisema kitendo cha watu kupotea katika mazingira tata linaweza kusababisha kushuka kwa uchumi kwani hakuna mwekezaji ambaye atavutiwa kuwekeza kwa kuhofia usalama wake.

Aliwataka viongozi wa dini kuhakikisha wanakemea vitendo hivyo kwa nguvu bila woga.

"Viongozi wa dini ni wazazi na ni jukumu letu kuhakikisha tunakemea, tunaonya na kupongeza pale mambo yatakapokuwa yameenda vizuri... sasa kama viongozi wa dini wanakwepa wamekaimisha madaraka yao kwa nani?" Alihoji Askofu mstaafu Mlyashimba.



Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, akizungumza na baadhi ya wafanyabiashara na wakazi wa Dodoma (hawapo pichani) kwenye uzinduzi wa hoteli ya kisasa ya Emirates jana. Kulia ni Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto na kushoto ni Shekhe wa Mkoa huo, Mustapha Rajabu.
**PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Watakiwa kuchukua tahadhari ya mvua

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WANANCHI wametakiwa kuendelea kuchukua tahadhari kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini.

Meneja wa Kanda ya Kati Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Izdori Kirenga, alisema mvua zinazoendelea kunyesha kwa sasa ni matokeo ya utabiri waliotoa kuanzia Oktoba, Novemba mwaka huu hadi Aprili, 2020, ambapo utabiri huo ulionyesha maeneo mengi yatapata mvua.

Kirenga alisema wananchi wanatakiwa kuchukua tahadhari za radi katika kipindi hiki cha mvua ili kujikinga na madhara yanayoweza kuzuilika.

Kadhalika, aliwataka wazazi na walezi kuchukua tahadhari kwa watoto katika kipindi hiki cha mvua na sikukuu za mwisho wa mwaka.

"Wazazi mnapaswa kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mvua kwa watoto kwa sababu mvua zinaendelea kunyesha kulingana na utabiri uliotolewa," alisema Kirenga. Alifafanua zaidi kuwa kinachotakiwa ni kujiandaa kisaikolojia na taarifa zinazotolewa na mamlaka husika juu ya utaratibu wa mvua ambazo zinanyesha.

Naye Sarah Mussa, mkazi wa jijini hapa alisema mvua zimekuwa za kushtukiza sana, hivyo wazazi wanapaswa kuwa makini kuziangalia familia husussani watoto kuwazuia wasiende maeneo hatarishi. Alisema wazazi wana kila sababu ya kuangalia familia na kusikiliza vyombo vya habari ili kujua taarifa mbalimbali za hali ya hewa.

Alisema kila siku serikali kupitia mamlaka zake imekuwa ikitangaza kuhusiana na mabadiliko ya tabia nchi hivyo ni vema wananchi tuyafuate.

# Madawati ya kijinsia 420 yaanza

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JUMLA ya madawati 420 ya jinsia yameanzishwa kwa ajili ya kuwezesha huduma stahiki kwa vituo vya polisi kutenda haki katika utatuzi wa ukatili wa kijinsia kisheria kwa waathirika wa matukio hayo.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni na Katibu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii Dk. John Jingu, wakati akitoa taarifa kuhusiana na mikakati iliyowekwa na serikali kwa ajili ya kupambana na ukatili wa kijinsia na rushwa ya ngono.

Dk. Jingu alisema mbali na hilo, wameanzisha vituo vinne vya mkono kwa mkono vya kutoa huduma kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia One Stop Center.

Alisema vituo hivyo vimelenga kufanya kazi ya kuwahudumia haraka waathirika wa vitendo vya ukatili na vinahusisha wataalamu mbalimbali ambao wamepata mafunzo kisheria ya namna ya kutatua changamoto zinazowakabiri waathirika wa ukatili wa kijinsia.

"Vituo hivi pia vinawezesha huduma za matibabu, unasihi na msaada wa kisheria," alisema Dk. Jingu.

Alisema ukiacha hilo serikali imetengeneza mtaala wenye kuzingatia masuala ya kijinsia wa mafunzo kwa wasaidizi wa kisheria ambapo hadi sasa watoa huduma 2,612 kutoka mikoa 26 wemeshapatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kusaidia waathirika.

Alisema kuanzishwa kwa vituo hivyo umekuwa msaada mkubwa katika maeneo mbalimbali kutokana na kwamba vimewasaidia kutatua changamoto mbalimbali ambazo zinajitokeza jamii za ukatili wa kijinsia.

Dk. Jingu alifafanua zaidi ya kuwa hizo zote ni jitihada ambazo zinafanywa na serikali ili kuhakikisha wanatokomeza ukatili wa kijinsia katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

"Ukatili wa kijinsia una madhara makubwa sana kwa jamii ndio maana unaona serikali imelivalia njuga sana suala hili ili kuhakikisha linatokomezwa," alisema Dk. Jingu.

Alisema kimsingi wanapopata fursa ya kujadili kwa kina namna ya kudhibiti vitendo vya kikatili ikiwamo kuyatafutia ufumbuzi masuala ya ukatili wa kijinsia.

Akitolea mfano katika vyuo vya elimu ya juu, alisema kumekuwa na mifumo dhaifu au kutokuwapo kabisa mifumo ya kushughulikia na kutokomeza ukatili wa kijinsia.

Alisema kamati za ulinzi za wanawake na watoto ambazo zimeanzishwa ni 11,520 katika ngazi zote kuanzia kitaifa hadi kijiji na mtaa.

Alifafanua zaidi kuwa katika kuhakikisha upatikanaji wa haki za wanawake na watoto hususan waathirika wa vitendo vya ukatili na katika utekelezaji wa sheria ya mwaka 2017 serikali imetengeneza mtaala wenye kuzingatia masuala ya jinsia wa mafunzo kwa wasaidizi wa kisheria.



## Kamati zatakiwa kutokomeza udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI zinazoshughulikia kesi za udhalilishaji wilayani zimetakiwa kujituma katika utendaji wa kazi zao ili ziweze kufanikiwa kutokomeza tatizo hilo.

Akizungumza katika kikao cha kutathmini utendaji wa kamati hizo Mwanakwerekwe, Meneja Sera na Utetezi wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania upande wa Zanzibar (Tamwa), Hawra Shamte, alisema, uzoefu unaonyesha kuwa kamati hizo hazifanyi kazi zao kwa umakini hali inayorudisha nyuma juhudi za kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa na mikakati mingi ya kuhakikisha vitendo vya udhalilishaji vinakomeshwa nchini, lakini bado vinazidi kuongezeka.

Vile vile, alisema ni vyema wajumbe wa kamati hizo wakatathmini juhudi hizo za serikali kukabiliana na janga hilo ambalo linarudisha nyuma ustawi wa jamii na maendeleo nchini. Wajumbe wa kamati hiyo, waliliomba Jeshi la Polisi kuielimisha jamii umuhimu wa kushirikiana kwa kuwapata wahalifu wa vitendo vya udhalilishaji ili kuondoa malalamiko ya wananchi kwa jeshi hilo. Walisema kuwa wananchi wengi hawafuatilii kesi zao na huishia kufutwa katika vituo vya polisi.

Juma Ali, miongoni mwa wajumbe wa kamati hizo, alisema katika kamati zao wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kutotumia wajumbe wa kamati katika vikao vyao jambo ambalo lengo la kuundwa kamati hizo kutotimia.

"Tunapofanya vikao mara nyingi wajumbe wa kamati, hawatumii na tunapojadili masuala yetu hayafiki kwa kuwa tunakuwa wachache sana," alisema.

Kikao hicho, kimepitia utekelezaji wa kamati hizo kwa kipindi cha Mei hadi Desemba 2019 na kumekuwa na ongezeko la kesi za ubakaji katika Wilaya ya Magharibi 'A' na Wilaya ya Kaskazini 'A'.

# Wapongezwa kwa kutoa elimu, afya bure

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VIONGOZI wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wamepongezwa kwa juhudi zao za kuendelea kutoa huduma muhimu za jamii kwa wananchi wake bure ikiwamo elimu na afya bure.

Akisoma salamu za Krismasi katika Kanisa la Minara Miwili, Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Zanzibar, Augustine Shao, alisema anaunga mkono juhudi zinazochukuliwa katika kuwapatia wananchi huduma muhimu za jamii.

Alisema mafanikio hayo yote yamekuja kwa kudhibiti fedha za umma na kupambana na ufisadi na rushwa katika sehemu za kazi.

"Serikali yetu imepiga hatua kubwa na kufanya mambo makubwa kwa maslahi ya taifa letu na tunajionea wananchi wanavyopata huduma za afya bure, elimu hadi ya msingi na sekondari," alisema.

Askofu Shao aliitaka Serikali ya Zanzibar kulipatia ufumbuzi tatizo la upatikanaji wa rasilimali ya mchanga ambalo limewafanya wananchi kushindwa kuendeleza shughuli zao za ujenzi na makazi.

Alisema kanisa linaunga mkono juhudi zinazochukuliwa katika kutunza mazingira na uharibifu wake ili kukifanya kisiwa cha Zanzibar kuwa salama, lakini kuwapo na njia mbadala ya kupata rasilimali ya mchanga.

"Lipo tatizo la uhaba wa mchanga linalowakabili wananchi wetu...tunataka lifanyiwe kazi huku suala la kutunza mazingira likizingatiwa kwa kiwango kikubwa," alisema.

Alisema nishati ya kuni na mkaa imekatazwa kwa sababu linaharibu mazingira kwa kukata miti ambayo ndio chanzo cha mvua, hivyo alitaka serikali kupunguza bei ya gesi na vyanzo vingine ili wananchi waache kutimia kuni na mkaa.



Mrajis wa Jumuiya zisizo za kiserikali, Ahmed Shaibu, akimkabidhi cheti Amina Miraji baada ya kumaliza mafunzo maalum ya wanawake watembeza watalii (Lady's tour guide) yaliofanyika mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# TTCL, PBZ kurahisisha huduma za kifedha

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Waziri Kindamba, amesema kuunganishwa kwa Shirika la TTCL kupitia kampuni yake ya T-PESA na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), itarahisishia wateja wao kufikia huduma za kifedha kwa njia ya simu.

Aliyasema hayo katika hafla ya uzinduzi wa huduma za kifedha kati ya shirika hilo la mawasiliano la TTCL kupitia T-PESA na Benki ya PBZ , mjini Unguja.

Alisema taasisi hizo zimeunganа zikiwa na lengo la kurahisisha wateja wao kupata huduma za kifedha kupitia njia ya simu.

Kadhalika alisema, kuwa shirika hilo linaendelea kufanya kazi zake vizuri, wamekuwa wakiboresha utekelezaji wa mipango yake mbalimbali katika utoaji wa huduma za simu za mezani, kiganjani na kupitia kampuni yake ya T-PESA.

"Hadi sasa T-PESA ambayo ni kampuni tanzu ya Shirika la Mawasiliano Tanzania TTCL, linazidi kuongeza huduma zake kwa wateja wake wa simu hadi nchi nzima na bila ya kuwaacha nyuma wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba," alisema.

Pia uboreshaji wa huduma za T-PESA umeleta ufanisi hasa kuongezeka kwa matumizi ya miamala ya ki-elektroniki kwa njia ya simu ambayo pamoja na uuzaji na ununuzi wa bidhaa ambao umezingatia usalama na unafuu wa huduma zinazotolewa. Alisema kampuni ya T-PESA imekuwa na dhamira ya kuwafikishia wananchi huduma za kifedha kwa njia ya kidijitali sehemu walipo ili kuokoa muda wao ambao wanautumia kuzalisha na kukuza uchumi.

"Fedha za dijitali ni ufikiaji wa huduma za elektroniki kwa njia ya miundombinu isiyo ya jadi ya benki (matawi ya ATM), hii inajumuisha utumiaji wa njia mbadala za kujiunga ambazo zinaendeshwa sana na teknolojia ya simu," alisema.

Kindamba alisema kuwa huduma hiyo itawawezesha wateja wote wa TTCL wenye akaunti ya T-PESA kutuma na kupokea fedha kwenye akaunti zao za PBZ kwa njia ya simu na pia wateja wa PBZ watalipia bili na kufanya miamala mbalimbali kwenda taasisi nyingine na kununua muda wa maongezi na vifurushi vya TTCL.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar, Juma Ameir Hafidh, alisema, ushirikiano huo, utarahisisha utoaji wa huduma na ushirikiano huo umeanza muda mrefu kwa kuuza floti kwa wateja wa T-PESA.

Alisema, mteja wa benki kwa sasa atahamisha pesa zake kupitia T-PESA na kupeleka benki kwa kila mteja anayetumia TTCL kupata huduma hizo kupitia kwa mawakala watakaokuwapo bila ya kwenda benki.

Alisema ushirikiano huo utawarahisishia wateja wao kwa kuwapa chaguo la kufanya shughuli za kibenki wakati wowote na saa yoyote wakiwa Tanzania.

# Wangabo asisitiza mshikamano KKKT

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, amesisitiza umoja na mshikamano kwa waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ambao kwa majuma kadhaa wamekuwa na mikwaruzano.

Hali iliwafanya waumini hao kusali kwa mafungu jambo ambalo, alisema halileti maendeleo ndani ya kanisa na mkoa.

Alisema kuwa alipoteuliwa na Rais John Magufuli na kuwasili katika mkoa huo, miongoni mwa viongozi wa dini waliomwombea ni Baba Askofu Ambele Mwaipopo ambaye anatambuliwa na serikali na kutahadharisha kuwa endapo serikali inamtambua kuwa ndio kiongozi wa kanisa hilo, iweje wanaushirika wasimtambue.

"Mimi niko ndani ya kanisa, nalitambua kanisa, namtambua Baba Askofu, kanisa hili limesajiliwa, Kanisa la Mungu, Baba Askofu wakati nilipofika tu hapa Mkoa wa Rukwa, Sumbawanga. Pamoja na viongozi wengine waliofika ofisini wakaniombea, Baba Askofu huyu alikuja akaniombea pia, wewe ni nani usiyemtambua?" Alihoji na kuendelea:

"Mimi niwatake na kuwaomba, wanausharika wote ambao wako nje ya kanisa warudi ndani ya kanisa."

Wangabo alisema kama waumini watashikamana Mungu huwa pamoja nao, na kamwe Mungu hawezi kumfuata mtu asiyependa umoja na kuwahakikishia kuwa wale wote ambao wapo nje ya kanisa kuwa Baba Askofu amekwisha wasamehe, hivyo wasiwe na sababu ya kuendelea kubaki nje ya kanisa.

Aidha, alisisitiza kuwa umoja kati ya waumini wa madhehebu mbalimbali ndani ya mkoa unachangia kwa kiasi kikubwa umoja wa wana-Rukwa, hivyo kusababisha mkoa kusonga mbele kimaendeleo.


Ameyasema hayo katika salamu zake za Krismasi juzi kwa wananchi wa mkoa huo, alizozitoa aliposhiriki ibada ya ya Krismasi katika kanisa la KKKT Dayosisi ya Ziwa Tanganyika.

Kwa upande wake Askofu Mwaipopo alimshukuru Wangabo kwa kutoa ujumbe mzuri wa mshikamano hasa katika siku ya kusherehekea kumbukumbu ya kuzaliwa Yesu Kristo, na kuwaomba waumini waliohudhuria ibada hiyo kuzungumza na wale wote waliopo nje ya kanisa hilo ili kuurudisha umoja na kupanga mambo ya kimaendeleo.

"Tukumbuke tuna mkakati mzuri kabisa wa kuandikwa wa dayosisi yetu ambayo tulikuwa tunayafanya, tumeweka kipaumbele, lakini baada ya mgogoro huu kwa kweli kulikuwa na kusimama mahala fulani."

"Lakini Mungu ni mwema hajatuacha, ndio maana shughuli hizi hapa kanisani zinaendelea, na tunashukuru sana kwa Mkuu wa Mkoa kututia moyo kwa ajili ya ujenzi wa kanisa hili."

Aliongeza kuwa pamoja na kuwa Mkuu wa Mkoa ni muumini wa Kanisa la Katoliki, lakini kwa upendo wake na kuguswa na jambo hilo, aliamua kusali pamoja na washirika wa Kanisa la KKKT.



Gari la watalii likiwa limesimama kumpisha twiga katika hifadhi mpya ya Taifa ya Burigi wilayani Chato mkoani Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tarura yamwibua mbunge barabara korofi

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MBUNGE wa Lulindi, Jerome Bwanausi, amepongeza Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara kuanza ujenzi wa barabara korofi ya Chiungutwa-Songambele yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 18.9.

Mbunge huyo alizitoa pongezi hizo juzi katika ziara ya ukaguzi wa barabara hizo na wajumbe wa bodi ya barabara ya wilaya ambayo iliongozana na watendaji wa Tarura.

Alisema barabara ya Chiungutwa-Songambele ni moja ya barabara korofi katika Jimbo la Lulindi, hivyo kusema kuwa Tarura kuamua kuijenga ni jambo la msingi.

Alisema barabara hiyo imekuwa ikitumiwa mara kwa mara na wananchi wa kata mbalimbali za Jimbo la Lilindi kwa shughuli za kiuchumi.

Bwanausi alisema barabara hiyo katika kipindi kama hiki cha masika haiwezekani kupitika kwa vile inakuwa imejaa tope, hivyo vyombo vya moto pamoja na baiskeli kushindwa kupita.

"Nawapongeza sana Tarura kwa kuamua kuijenga barabara hii na zingine zote katika jimbo langu... kwa kweli barabara hii itawasaidia sana wananchi ikikamilika," alisema Bwanausi.

Aidha, alisema Tarura inapaswa kusimamia vema miradi yote inayoitekeleza katika maeneo mbalimbali ya jimbo hilo ili iweze kukamilika kwa wakati na kuleta tija kwa wananchi.

Alisema licha ya wakala huo kuanza kufanya ujenzi wa barabara hizo, lakini unapaswa kuangalia uwezekano kuzifanyia matengenezo barabara zingine ambazo ni korofi katika jimbo hilo.

Meneja wa Tarura Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Wiliam Tizalwa, alisema katika bajeti ya 2019/2020 ya matengenezo ya barabara imekusudia barabara zote korofi kuzifanyia maboresho. Alisema kadri bajeti itakavyokuwa ikiruhusu, ndivyo barabara hizo zitakavyokuwa zikifanyiwa maboresho ili zote ziwe katika ubora.

Alisema barabara ya Chiungutwa-Songambele inatengenezwa na mkandarasi mzawa ambaye ni DEELCOM Tanzania LTD kwa gharama ya Sh. milioni 18.9.

Barabara zingine ambazo Tarura inazifanyia maboresho ni Ndanda-Miyuyu kwa Sh. milioni 39.1, Ruangwa-Ndanda kwa Sh. milioni 15.9, Ndanda-Miyuyu kwa Sh. milioni 55.9 na Likanga-Nambarapi kwa Sh. milioni 65.9.

# Wahitimu mafunzo mgambo wafundwa

Na Hamisi Nasiri, MTWARA

WAHITIMU wa mafunzo ya mgambo wilayani Newala mkoani Mtwara, wametakiwa kuyatumia vizuri mafunzo waliyoyapata kwa kuwa mabalozi wema katika jamii ili kudumisha amani na usalama.

Wito huo ulitolewa wilayani Newala na Mkuu wa Wilaya hiyo, Aziza Mangosongo, kwenye sherehe za kuhitimisha mafunzo ya Jeshi la Akiba Mgambo.

Mangosongo ambaye alikuwa mgeni rasmi katika sherehe hizo, alisema wahitimu hao wanapaswa kutumia vema mafunzo waliyoyapata kwa kuepukana na vitendo vya uhalifu bali wachukue mafunzo hayo kulinda amani ya Tanzania.

Alisema hakutakuwa na umuhimu wowote kwa vijana hao kuhitimu mfunzo hayo kisha kuingia katika jamii na kufanya mambo ambayo hayaendani na umuhimu wa wao kupata mafunzo hayo.

Mangosongo alisema lengo la kwanza la serikali kutoa mafunzo hayo kwa vijana mbalimbali ni kuwajengea uzalendo kwa taifa lao.

Alisema wahitimu wa mafuzo hayo ni lazima waweke mbele utaifa wao na uzalendo kwa kufanya mambo mema kupitia mafunzo waliyo yapata.

Mangosongo alisema haitakuwa vizuri iwapo vijana hao wataingia katika jamii kufanya vurugu, uvunjifu wa amani kwa vile wana ujuzi wa kijeshi.

"Naomba vijana myatumie vizuri mafunzo mliyoyapata na msije kwenda huko katika jamii mkafanya mambo yasiyopendeza, dumisheni amani na uzalendo," alisema Mangosongo.

Aidha, Mangosongo aliwataka viongozi mbalimbali wilayani humo na jamii kwa ujumla kuwahamisha vijana wa kike kujiunga na mafunzo hayo kwani mwamko bado umekuwa mdogo.

Naye mshauri wa mgambo wilayani Newala, Meja Lugongo, alisema lengo kubwa la mafunzo hayo ni kuwawezesha vijana hao uelewa wa dhana nzima ya ulinzi wa umma na maudhui yake, vile vile kuwa tegemeo la nchi katika masuala ya ulinzi kwenye maeneo yao.

Wahitimu wa mafunzo hayo kupitia risala yao, waliahidi kuwa yote waliyofundishwa watayazingatia na kufanyia kazi kwa manufaa ya taifa.

# Mbunge Republican akerwa na msimamo wa wenzake



**WASHINGTON,** Marekani

SENETA wa Republican Lisa Murkowski (pichani), amesema kwamba amekerwa na msimamo wa chama chake kabla ya kusikilizwa kesi inayomkabili Rais Donald Trump, kuwasilishwa katika bunge hilo.

Rais Trump, alishtakiwa katika Bunge la Uwakilishi linalotawaliwa na wabunge wa Democrat kwa utumizi mbaya wa mamlaka na kulizuia Bunge la Congress kufanya kazi.

Kwa sasa anakabiliwa na kesi hiyo katika Bunge la Seneti linalotawaliwa na wanachama wengi wa Chama cha Republican.

Hata hivyo seneta wa walio wengi katika bunge hilo la seneta Mitch McConnel, ameahidi kushirikiana na ikulu ya White House. Trump, amekuwa rais wa tatu kushtakiwa katika mabunge hayo, hata hivyo hakuna uwezekano wa kumwondoa madarakani kutokana na wingi wa Republicans katika bunge hilo.

Rais huyo ametaja mchakato wa kesi hiyo kama uwindaji wa kisiasa.

Hata hivyo, amekiambia kituo cha habari cha Alaska (KTUU) kwamba hafurahii jinsi McConnel anavyotoa matamshi ya ushirikiano na Ikulu ya Whitehouse.

"Niliposikia hilo nilikerwa sana," alisema.

Seneta huyo pia alisema kunahitajika kuwepo na uwazi na kutoshirikiana kati ya Bunge la Seneti na Ikulu ya Whitehouse kuhusu jinsi kesi hiyo itakavyoandaliwa.

"Kwangu mimi inamaanisha kwamba tunahitaji kurudi nyuma na kutopendelea upande unaojitetea," alisema.

Hata hivyo Murkowski, mwanachama wa Republican mwenye msimamo wa kadri, amemkosoa Trump kuhusu sera kadhaa. **BBC**

## Rais Burkina Faso atangaza maombolezo

**OUAGADOUGOU,** Burkina Faso

RAIS wa Burkina Faso, Roch Marc Christian Kabore (pichani chini), ametangaza siku mbili za maombolezo kufuatia mashambulizi yaliyofanywa na wanamgambo wenye itikadi kali na kuwaua watu 35.

Mashambulizi hayo ya juzi yalitokea katika mji wa Arbinda.

Rais Kabore, amesema wanamgambo 80 waliuawa baada ya makabiliano ya saa kadhaa na vikosi vya usalama katika eneo hilo karibu na mpaka na Mali.

Kulingana na taarifa ya jeshi, maofisa saba wa vikosi vya usalama, waliokuwa miongoni mwa waliokabiliana na wanamgambo hao waliuawa. Mashambulizi ya wanamgambo hutokea mara kwa mara katika eneo hilo, lakini idadi ya waliouawa wakati huu ni ya juu zaidi.

Hakuna kundi lolote ambalo limedai kuhusika na mashambulizi hayo.

Burkina Faso ambayo hupakana na Mali na Niger imeshuhudia mashambulizi mengi ambayo yamesababisha vifo vya mamia ya watu tangu mwanzo wa mwaka 2015, wakati mashambulizi ya wanamgambo yalipoanza kuenea katika ukanda huo wa Sahel. **DW**





Soko la Krismasi la Berlin, Ujerumani ni moja ya kivutio wakati wa shamrashamra za sherehe hiyo ya kuzaliwa Yesu Kristo. Maadhimisho hayo yalifanyika juzi. **PICHA: AP**

## Treni zakosesha watu kufurahia Krismasi

**PARIS,** Ufaransa

SIKUKUU ya Krismasi haikuleta jibu kwa wasafiri nchini Ufaransa, wakati mgomo wa usafiri ukiingia katika wiki ya nne, na kuharibu safari za maelfu ya watu waliotaka kusafiri kusherehekea na ndugu zao.

Watu wengi wamehangaika katika dakika za mwisho kutafuta njia mbadala wakati maandamano dhidi ya mageuzi ya pensheni yakiendelea.

Treni zilifuta au kuchelewesha safari , huku teksi, huduma za kusafiri na wenye magari na mashirika ya magari ya kukodi yakiziba nafasi hiyo ya upungufu wa treni.

Maelfu ya watu wamekosa huduma ya usafiri wakati huu wa sherehe za Krismasi katika miji mingi nchini Ufaransa.

Ni sehemu ndogo tu ya treni za mwendo kasi na treni zinazosafiri kati ya miji mikuu zilifanya kazi katika mkesha wa sikukuu ya Krismasi na hata treni chache zaidi zilifanyakazi.

Wakati wa shamra shamra zenyewe hapo juzi, vituo vikuu vya treni mjini Paris vilifungwa majira ya asubuhi ambapo huduma za kwenda maeneo ya mashambani zilipunguzwa.

Rais Emmanuel Macron, alitoa wito wa kuwapo na suluhu wakati huu wa sikukuu , lakini majadiliano kati ya serikali na vyama vya wafanyakazi wiki iliyopita yalishindwa kupata msimamo wa pamoja. **DW**

## Papa Francis ataka matumaini dhidi giza

**VATICAN CITY,** Vatican

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, ametoa ujumbe wa Krismasi akizungumzia matumaini dhidi ya giza linaloikumba ulimwengu.

Alisema giza hilo linatokana na machafuko na mahusiano mabaya katika sehemu mbalimbali kuanzia Mashariki ya Kati, Amerika hadi Afrika. Papa Francis aliwaambia maelfu ya watu wakiwamo watalii, mahujaji na wenyeji wa mji wa Rome waliokusanyika katika eneo la Kanisa la Mtakatifu Petro kuusikiliza ujumbe wake wa kila mwaka wa Krismasi.

Alisema kwamba nuru ya Kristo ni kubwa kuliko giza katika mioyo ya wanadamu, na katika mivutano ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Alitoa mfano wa Wasyria ambao hawaoni dalili ya kumalizika kwa uhasama ambao umesababisha machafuko nchini mwao kwa miaka mingi. **DW**

# H'shauri yadaiwa kushindwa kukusanya hata shilingi

**Na Boniface Gideon,** KOROGWE

MBUNGE wa Jimbo la Korogwe Vijijini, Timotheo Mnzava na madiwani, wameishauri Halmashauri ya Korogwe kuongeza nguvu ya ukusanyaji wa mapato hususani ya minada ya mifugo.

Wakizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani, walisema katika taarifa ya ukusanyaji mapato ya minada kwa mwezi Juni na Julai, mwaka huu wataalamu wa halmashauri hiyo hawakufanikiwa kukusanya hata shilingi moja, huku mwezi Agosti hadi Novemba taarifa zikionyesha walikusanya Sh. 99,000 hali ambayo inaashiria kuwa na upigaji wa pesa za umma.

Seif Hilal, Diwani wa Mashewa na Aweso Kipaku, Diwani wa Mswaha, waliitaka halmashauri hiyo kuwachukulia hatua kali watendaji wote waliohusika na sakata la utakatishaji fedha za mapato ya minada. "Hapa kunatakiwa kuchukuliwe hatua kali ikiwezekana wakamatwe leo leo," alisisitiza Kipaku.

Naye Seif Hilal, Diwani wa Mashewa, alisema mnada mmoja kwa siku una uwezo wa kuingiza zaidi ya ng'ombe 300, hivyo wanashangaa kuona makusanyo ya mapato ni kidogo na wakati mwingine hawakusanyi kabisa.

Katika kikao hicho madiwani walionyesha kutofurahishwa na utendaji kazi wa watendaji kitengo cha ukusanyaji mapato kutokana na kuwa na kasoro nyingi kwenye taarifa na upigaji pesa kwa kujaza taarifa za uongo.

Naye Mbunge wa Jimbo hilo, Timotheo Mnzava, alimwomba Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Kwame Daftari, kuwaagiza watendaji hao kupeleka taarifa kwenye Baraza la Madiwani lijalo mwezi Januari 2020, na taarifa hiyo isomwe.

"Naomba madiwani tutulie ili kwenye baraza lijalo watueleze kila kitu naamini tutapata ukweli wa hili," alisema Mnzava.



Wanawake wa Kijiji na Kata ya Isaka, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wakiwa wamekalia vyerehani walivyopatiwa bure na Jumuiya ya International Istiqaama Muslimu Community, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Walilia serikali kujenga kituo uangalizi wanawake waathirika dawa za kulevya

**Na Dege Masoli,** TANGA

WAATHIRIKA wa dawa za kulevya mkoani hapa wamefunga mwaka kwa kuiomba serikali kupelekewa huduma ya dawa ya methadone na kujengewa 'sober house' (kituo cha uangalizi) kwa ajili ya wanawake.

Wakizungumza wakati wa sherehe ya kuadhimisha Sikukuu ya Krismasi iliyofanyika juzi katika Kanisa la Glory Land lililopo uwanja wa Sabasaba jijini hapa, walieleza kuwa dawa hiyo inahitajika kwa kiwango kikubwa hasa kwa waliopata maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Mratibu wa Asasi ya kiraia ya Gift of Hope, jijini hapa inayotunza watu walioathirika na dawa za kulevya, Said Bandawe, alieleza kuwa wenye maambukizi ya Ukimwi wakitumia dawa za kufubaza virusi hivyo (ARV) mara nyingi huwa siyo wafuasi wazuri wa kuzingatia tiba hizo.

Bandawe alisema kuwapo kwa dawa ya methadone kutasaidia walengwa kuitumia dawa hiyo kama mbadala wa heroin na hivyo kudhibiti hali za afya yao kwa kuzingatia matumizi ya dawa hizo.

Naye Bakari Abeid, alitoa angalizo kwa wadau wa kudhibiti dawa za kulevya kusimamia kwa umakini suala la matumizi ya dawa hizo ili kunusuru jamii na kizazi kilichopo. Kwa upande wake Abdalah Mwakinyo, ambaye ni msimamizi wa kituo hicho, alielezea manufaa ya kupatikana kwa methadone kutakavyo wezesha watu walio mitaani na ambao hawajafikiwa na huduma za sober house kuepukana na athari hizo.

Akizungumza katika sherehe hizo, Mchungaji Manase Maganga, anayeongoza kanisa hilo, alisema wanawake wengi wameathirika na dawa za kulevya, lakini changamoto kubwa ni ukosefu wa sober house yao, huku akiomba serikali kulipa kipaumbele suala hilo ili kuwapatia huduma wanawake hao.

Manase alieleza kuwa jamii ni lazima itambue kuwa watumiaji wa dawa za kulevya siyo waovu bali walianza matumizi hayo kama mchezo na wanahitaji msaada wa kuwaokoa.

Hata hivyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, alielezea umuhimu wa kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu ili kuokoka na kuwa raia wema kama ilivyokuwa awali.

Kanisa la Gloryland limesherehekea Sikukuu ya Krismasi kwa pamoja na kushirikisha makundi ya wajane, yatima, waathirika wa dawa za kulevya, wenye ulemavu, pamoja na wazee wasiojiweza na kutoa misaada ya vifaa mbalimbali ikiwamo vyakula.

# Watoto 50 mazingira magumu kukatiwa bima

**Na Dege Masoli,** KOROGWE

TAASISI ya Korogwe Community Foundation iliyopo wilayani hapa imejipanga kuwakatia bima ya afya watoto zaidi ya 50 wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi wilayani humo.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Magasa Sijjo aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa taasisi hiyo uliofanyika mjini Korogwe na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo wa kiserikali na jamii.

Alisema pamoja na mambo mengine wamejipanga kuelekeza nguvu zao kuwasaidia watoto walio katika mazingira magumu na hatarishi maeneo yote ya Wilaya ya Korogwe.

Sijjo alisema taasisi hiyo inajihusisha na kuwasaidia watoto hao katika masuala ya kugharamia mahitaji ya elimu na afya kwa upande wa matibabu na kuboresha huduma zake imejiandaa kwa kugawa kadi za bima ya afya kwa watoto wapatao 50 kuanzia Januari, 2020.

"Tutagawa kadi hizo lengo ni kuwasaidia watoto hao ambao miongoni mwao ni yatima na wanauhitaji mkubwa wa kupewa misaada muhimu ya kibinadamu kama ilivyo kwa wenzao wengine...kwa kuanzia tutatoa kadi 50," alisema Sijjo.

Alifafanua kuwa taasisi hiyo inaanzia kutoa huduma zake kwa watoto wa Wilaya ya Korogwe, huku lengo likiwa ni kuwafikia pia waliyopo kwenye wilaya nyingine za Mkoa wa Tanga.

Aliiomba serikali kutanua wigo wa kutoa ruzuku kwa taasisi zote zinazojihusisha na kusaidia watoto wenye mahitaji maalumu na waliyopo kwenye mazingira hatarishi ili kuziongezea nguvu ya kuihudumia jamii hiyo.

Alieleza kuwa kufanya hivyo kutazifanya taasisi hiyo kudumu bila kutegemea wahisani ambao mara nyingi huishia njiani na kusababisha huduma hizo kukoma na watoto hao kurejea tena maisha ya awali.

Alitoa wito kwa viongozi wa kidini kutochoka kuliombea taifa na viongozi wake waongoze nchi kwa haki ili amani, upendo na mshikamano udumu kwa kila mmoja kupata anachokistahili na kufaidi matunda ya taifa.

# HABARI PICHA



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakiwa kwenye ufukwe wa Coco, yakiwa ni maadhimisho sikukuu ya Krismasi na 'Boxing Day'. **PICHA ZOTE: SELEMANI MPOCHI**



Watoto wakivalishana mpira kwa ajili ya kuogelea katika ufukwe wa Coco.



Wakazi wa Jiji wakiogelea katika ufukwe wa Coco jana.



Vijana wakirudisha mipira waliyokodi baada ya kuogelea, jana.



Wakazi wa Jiji wakiogelea.



Kijana aliyekodisha kifaa cha kuogelea akikitoa kwenye maji.

## HABARI MICHEZO



# LUKAKU: POGBA ALIJUA NAONDOKA UNITED

**MILAN,** Italia

ROMELU Lukaku amefichua kwamba mtu wa kwanza kwenye kikosi cha Manchester United kumwambia kwamba anaondoka ni Paul Pogba.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alisema kwamba alichoshwa na vitendo vya kukosolewa tu yeye kwa muda wake wote alipokuwa Old Trafford.

Kutokana na hilo, Lukaku aliamua kuondoka zake kwenda kujiunga na Inter Milan kwenye dirisha lililopita la majira ya joto kwa pauni milioni 73 na tangu wakati huo amefunga mabao 12 katika mechi 17 alizocheza kwenye Serie A na kuisaidia timu kuongoza ligi.

Man United huko kwa upande wao wanawaza kumsajili mshambuliaji mwingine wa kuja kuziba pengo lake katika dirisha la Januari na wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kumnasa staa wa Red Bull Salzburg, Erling Haaland.

Lukaku alifunga mabao 42 katika mechi 96 za michuano yote alizoitumikia Man United kwa misimu miwili, lakini anadhani mashabiki waliokuwa wakitazama zaidi nafasi alizokuwa akikosa kuliko alizofunga.

Alichofanya alimwambia swahiba wake, Pogba kwamba anaondoka wakati walipokuwa wakielekea kwenye maandalizi ya msimu mpya huko Australia.

"Nilimwambia, nimechoka," alisema Lukaku.

# Arteta: Ljungberg atakuwa msaidizi wangu

**LONDON,** England

KOCHA mpya wa Arsenal, Mikel Arteta, amemtaja, Freddie Ljungberg, ataendelea kuwa msaidizi wake kwenye kikosi hicho cha timu hiyo.


Kiungo huyo wa pembeni wa zamani wa Arsenal, Ljungberg, aliisimamia timu hiyo katika mechi sita akiwa kocha wa muda baada ya Unai Emery kufutwa kazi kutokana na kufanya ovyo na kuvuna matokeo mabaya.

Ljungberg alishinda mechi moja tu, 3-1 alipowachapa West Ham United na mechi yake ya mwisho ilimalizika kwa sare ya bila kufungana dhidi ya Everton Jumamosi iliyopita.

Arteta alikuwa jukwaani Goodison Park kutazama mechi hiyo sambamba na Mkurugenzi wa Ufundi, Edu na Steve Round, ambaye atakuwa kocha msaidizi.

Round alikuwa kocha wa Middlesbrough, Newcastle United, Everton, Manchester United na England na alikuwa mkurugenzi wa soka katika klabu ya Aston Villa.

Kwenye orodha ya wasaidizi watatu, mwingine ni Albert Stuivenberg, ambaye aliwahi kuwa msaidizi wa Louis van Gaal huko Old Trafford.






# Lampard asema Mourinho alikosea kuuza nyota Chelsea

**LONDON,** England

FRANK Lampard amempiga kijembe, Jose Mourinho akiponda uamuzi wake wa kuwaacha Kevin De Bruyne na Mohamed Salah waondoke Stamford Bridge.

Mourinho, ambaye kwa sasa ni kocha wa Tottenham Hotspur alifanya kazi na nyota hao wawili katika kipindi chake cha pili alichokuwa kwenye kikosi cha Chelsea. Lakini, wachezaji wote hao walionekana kuwa hawajui na kuondoshwa kwenye timu.

De Bruyne aliuzwa kwenda Wolfsburg kwa ada ya pauni milioni 18 mwaka 2014 na Salah alienda AS Roma mwaka 2016 kwa ada ya pauni milioni 12.

Baadaye wakarudi kwenye Ligi Kuu England, Bruyne akitua Manchester City na Mo Salah akisaini Liverpool, ambapo kwa sasa wamekuwa mastaa wakubwa sana kwenye timu hizo na kutamba huku Chelsea wakiishia tu kukodoa macho.

Lampard, ambaye Jumapili iliyopita alimchapa kocha wake huyo wa zamani, Mourinho mabao 2-0, timu zao zilipokutana kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, alimpiga kijembe Mreno huyo akisema: "Kama ungekuwa makini na kujali mambo yako basi tungekuwa na timu ya wachezaji wazuri na kuendelea kutamba hadi sasa.

# Barca kusajili wapya wawili

**BARCELONA,** Hispania

KATIKA kuendelea kuimarisha kikosi chake, Barcelona imeanza mpango wa kusajili wachezaji wawili wapya, ambao mmoja atakuwa ni kiungo mchezeshaji na mwingine ni mshambuliaji wa kati.

Inaelezwa kuwa ili benchi la ufundi la vinara hao wa La Liga liweze kuwa na amani, linahitaji kuongeza nguvu kwenye idara hizo.

Gazeti la Hispania la kila siku limeandika kuwa, nyota wanaowindwa na Barcelona ni pamoja na Doyell Malen wa PSV Eindhoven na Lautaro Martinez wa Inter Milan.

Imeandikwa kuwa Kocha Ernesto Valverde amekuwa akivutiwa zaidi na kiwango cha Martinez na huenda anachukua nafasi ya Sergio Busquets, ambaye ameshaitumikia kwa muda mrefu timu hiyo.

Martinez (22), amefunga mabao 11 katika mechi 18 alizoichezea Inter msimu huu, wakati nyota aliyeanzia Arsenal, Malen (20), amepachika wavuni mabao 11 katika michezo 14 ambayo amecheza katika ligi hiyo maarufu Eredivisie. Pia kiungo Stephano Sensi, anatakwa kuivutia klabu hiyo ya San Siro akiwa kwa mkopo kutoka Sassuolo.



# MANDZUKIC RASMI AJIUNGA AL-DUHAIL



**TURIN,** Italia

KLABU ya Al-Duhail imethibitisha kwamba imemsajili Mario Mandzukic kutoka Juventus.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia alishinda mataji manne ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A na kombe la Coppa Italia mara tatu wakati akicheza kwa misimu minne na nusu pale Turin.

Hata hivyo, Mandzukic ameonekana kukosa namba kwenye kikosi cha Juve chini ya kocha, Maurizio Sarri msimu huu, na aliachwa kwenye kikosi cha Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Awali alihusishwa na mpango wa kuhamia Manchester United, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 ameamua kuhamia kule Qatar kuendelea kucheza soka.

Wakati Juventus hakikutangaza haraka kuondoka kwake, Al-Duhail iliweka picha kwenye ukurasa wake wa Twitter na kusema imemsajili mchezaji huyo.

Hata hivyo, hakuna maelezo zaidi juu ya uhamisho wake na kiasi gani cha fedha kimetumika.

Mandzukic alikuwa kwenye kiwango bora wakati Croatia ikishika nafasi ya pili kwenye michuano ya Kombe la Dunia nchini Urusi na alifunga mabao matatu.

Kabla ya kujiunga na Juventus, mshambuliaji huyo alicheza kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, akiwa na Bayern Munich na baadaye Wolfsburg, pamoja na kucheza msimu mmoja pale Atletico Madrid.

# *Arsenal yajipanga kumsajili Gabriel*

**LONDON,** England

KOCHA mpya wa Arsenal, Mikel Arteta, ameanza mipango ya kuimarisha kikosi chake na sasa ameweka wazi kwamba anahitaji saini ya beki wa Lille, Gabriel.

Mhispania huyo tayari ameanza mchakato wa kuhakikisha beki huyo anatua klabuni kwake na hatimaye anaimarisha safu yake ya ulinzi na kuirejesha Arsenal kwenye soka la ushindani.

Hata hivyo, Arteta, anaonekana kukwama katika mchakato mwingine wa kumsajili beki wa Napoli, Kalidou Koulibaly, baada ya kuelezwa kufuata historia ya klabu hiyo kwenye matumizi ya fedha, hasa kutokana na matumizi wanayotarajia kufanya mwakani kwenye kipindi cha majira ya joto.

Uwezekano na dau la kumsajili Gabriel linaonekana kuwa rahisi ukilinganisha na Koulibaly, huku pia Mbrazili huyo mwenye umri wa miaka 22, akionyesha kiwango kizuri kwenye mechi zote 23 alizoichezea Lille msimu huu.

Kati ya mechi hiyo, sita zilikuwa za Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini kujumuishwa kwake kwenye mechi za kuwania tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki katika kikosi cha vijana wa umri chini ya miaka 23 cha Brazil mapema mwezi ujao, kinaweza kukwamisha zoezi hilo kukamilika mapema.

Mkataba wa nyota huyo wa zamani wa Dinamo Zagreb ambaye anaichezea kwa mkopo klabu hiyo inayoshiriki Ligue 1 umebakiza miezi 18, na inamaanisha kuwa Arsenal wanaweza kuwa kwenye nafasi kufanya mazungumzo marefu mwezi ujao.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# COUTINHO AFIKIRIA KUREJEA ENGLAND

## ●●● Ni endapo Bayern Munich itakataa kumpa mkataba wa muda mrefu...

**MUNICH,** Ujerumani

PHILIPPE Coutinho amebainisha kuwa anafikiria kurudi kwenye Ligi Kuu England mwakani kama Bayern Munich hawatampa mkataba wa kudumu.

Barcelona walimpeleka Coutinho kwa mkopo Bayern Munich kwa mkataba wa msimu mmmoja, huku kukiwa na makubaliano ya kumsajili kwa kumpa mkataba wa kudumu kama watapendezwa naye itakapofika mwisho wa msimu.

Mbrazili huyo anajaribu kucheza soka la kiwango cha juu kuwashawishi Bayern ili kufungua pochi kumnasa jumla ambapo bei yake inatajwa kuwa ni Euro milioni 120.

**Lakini, wasiwasi uliopo ni kama Bayern Munich watakuwa tayari kutoa kiasi hicho cha fedha kumsajili Mbrazili huyo wakati kuna wachezaji wengine wanaocheza kwenye nafasi kama ya Coutinho, na wanapatikana kwa bei ndogo zaidi.**

Kama dili la kubaki Allianz Arena litakwama, ripoti zinadai kwamba Coutinho atafungua milango ya kurudi England, huku klabu za Manchester United na Tottenham Hotspur zikionyesha dhamira ya kunasa huduma yake tangu dirisha lililopita la majira ya kiangazi.

Mastaa wa Bayern Munich wamewataka mabosi wao kuhakikisha wanamsajili jumla Coutinho.

Chelsea nao wamedaiwa kuhitaji saini ya mchezaji huyo na wanaamini kwamba watawashawishi Barcelona wamsajili dau la pauni milioni 86 tu. Hata hivyo, mpango wa kwanza wa Coutinho ni kubaki Bayern Munich.

"Nimetulizana hapa. Mpango wangu ni kubaki hapa, na nimeelekeza akili yangu kubaki hapa," alisema.

## ZISIKUPITE

### MADDISON KUIGHARIMU UNITED

MANCHESTER United inatarajia kuweka dau la pauni milioni 80 kwa ajili ya kuwania saini ya kiungo wa Leicester na Timu ya Taifa ya England, James Maddison, ambaye ana umri wa miaka 23, katika kipindi cha majira ya joto. ***(Daily Star)***

### TODIBO AGOMBEWA ULAYA

MONACO imeungana na AC Milan pamoja na Manchester United katika vita ya kuwania saini ya beki wa kati wa Barcelona Mfaransa Jean-Clair Todibo, ambaye ana umri wa miaka 19. ***(Calciomercato)***

### PELLEGRINI KUSAJILI WANNE

KOCHA wa West Ham, Manuel Pellegrini, ambaye amekalia kuti kavu katika Ligi Kuu England, amesema kuwa anahitaji kusajili wachezaji wapya wanne kwenye dirisha dogo la Januari, lakini yuko tayari pia kumwania beki, Issa Diop (22), kuondoka klabuni hapo. ***(Express)***

### CAVANI MAMBO SAFI

STRAIKA wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani, ambaye ana umri wa miaka 32, anakaribia kukamilisha mchakato wa kujiunga na Atletico Madrid katika kipindi cha dirisha dogo la Januari. ***(Marca)***

### VILLA KUMKOSA RASHICA

ASTON Villa inaonekana kukata tamaa ya kupata saini ya winga wa Werder Bremen na Timu ya Taifa ya Kosovo, Milot Rashica, ambaye ana umri wa miaka 23 kutokana na kutakiwa kulipa kiasi kikubwa cha ada. Villa ilitaka kumsajili nyota huyo katika dirisha dogo la Januari. ***(Birmingham Mail)***

### JESUS AITUNUKU FLAMENGO

KOCHA wa Flamengo, Jorge Jesus, amesema kuwa anatarajia kutoa kwa heshima mkataba wake na klabu hiyo ya Brazil baada ya kufanikiwa kutinga hatua ya fainali ya Klabu Bingwa ya Dunia. ***(Record - in Portuguese)***

### LIVERPOOL WAANZA NYODO

LIVERPOOL inataka kuomba ruhusa kwa Bodi ya Ligi Kuu England ya kuvaa jezi zenye nembo ya taji la Klabu Bingwa ya Dunia katika mechi zao za ligi wanazocheza. ***(The Athletic - subscription required)***

### CITY YAMWANIA IHATTAREN

MANCHESTER City imeweka wazi nia yake ya kumwania kiungo wa PSV Eindhoven, Mohamed Ihattaren, ambaye msimu huu amejihakikishia namba katika kikosi cha kwanza cha Eredivisie. Yosso huyo mwenye umri wa miaka 17 anaamini nyota huyo atarithi mikoba ya David Silva, ambaye anajiandaa kuondoka Etihad mwishoni mwa msimu. ***(Sun)***

### ZAZA ATAJWA FIORENTINA

MABOSI wa Fiorentina wameanza mchakato wa kumwania straika wa Torino, Simone Zaza, lakini Calciomercato watakumbana na ushindani kutoka kwa klabu mbalimbali za La Liga, ikiwamo Sevilla na Espanyol kumnasa nyota huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Sun)***

### ALENA ANUKIA BARCA

BARCELONA imejipanga kumsajili, Carles Alena katika kipindi cha dirisha dogo la Januari. Nyota huyo pamoja na Todibo (19), wanawaniwa pia na Getafe na Real Betis. ***(Marca)***

HABARI MICHEZO

# KOCHA LIPULI AKIRI SIMBA HAIKAMATIKI

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya timu yake kupata kichapo cha mabao 4-0, Kocha Mkuu wa Lipuli FC, Haruna Hassan, amesema kuwa kikosi chake kilikosa umakini na kusababisha kupoteza mchezo huo dhidi ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, ambao ulichezwa jijini Dar es Salaam juzi.

**Katika mchezo huo uliochezeshwa na mwamuzi, Martin Saanya, kutoka Morogoro, Simba ilienda mapumziko ikiwa inaongoza kwa bao 1-0.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Haruna, alisema kuwa hajaridhishwa na hakuridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mchezo huo.

Haruna alisema kuwa kutofuata maelekezo na kupoteza umakini, ni moja ya sababu zilizopelekea kupoteza mechi hiyo ya ugenini.

"Sijafurahishwa na matokeo tuliyoyapata, vijana wangu wameniangusha sana, walichokifanya uwanjani ni tofauti na maelekezo niliyowapa, ila ndio mchezo wa soka ulivyo, ukifanya kosa, mpinzani wako analitumia kupata faida," alisema Haruna.

Aliongeza kuwa bado ana nafasi ya kurekebisha upungufu wote uliojitokeza ili kuhakikisha timu hiyo inaendelea kubakia kwenye ligi hiyo ya juu Tanzania Bara.

"Nitayafanyia kazi makosa yote niliyoyabaini ili kujihami na kushuka daraja, tutatumia nguvu zaidi ili tubakie kwenye Ligi Kuu," Haruna alisema.

Naye nahodha wa Lipuli, Paul Nonga, alisema kuwa kikosi chao kilicheza tofauti na malengo waliyojiandaa nayo, lakini wanarudi Iringa ili kujipanga upya na mechi zinazofuata.

"Tumeruhusu magoli mepesi sana, tumefanya makosa ambayo wapinzani wetu wameyatumia, mwisho wa mchezo huu, ndio mwanzo wa maandalizi ya mchezo unaofuata, tunarudi nyumbani, tutapambana kusaka ushindi," alisema Nonga.



Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya ukiwa katika hali mbaya baada ya kumalizika kwa tamasha la muziki wa kizazi kipya lililofanyika juzi. Tamasha hilo lilikuwa la bure. **PICHAI ISAAC KIJOTI**

# Kagere afurahia kucheka na nyavu




**Na Shufaa Lyimo**

MSHAMBULIAJI wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Meddie Kagere, amesema kuwa anafurahi kuona timu yake imepata ushindi mnono dhidi ya Lipuli FC na kuendelea kujiimarisha kutetea taji hilo.

Kagere ambaye alifunga bao moja katika ushindi wa magoli 4-0, alisema kuwa matokeo hayo yalimfanya asherehekee sikukuu ya Krismasi vema.

"Sikukuu kwa upande wangu ilikuwa nzuri kwa sababu timu yangu ilishinda mchezo wetu kwa kufunga mabao 4-0, ilikuwa ni furaha ya aina yake," alisema Kagere.

Mnyarwanda huyo alisema lengo ni kuendelea kujituma zaidi ili kuhakikisha wanatetea ubingwa mapema na wanawashukuru mashabiki wao kwa ushirikiano wanaowapa.

"Tunawashukuru mashabiki wetu kwa ushirikiano wanaotupa kwa kujitokeza kwa wingi uwanjani tunapokuwa tunacheza, hii inatupa nguvu zaidi ya kupambana, " alisema Kagere.

Simba inatarajia kushuka tena dimbani kesho kuwavaa KMC FC kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

## Polisi Tanzania yajitabiria mazuri

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Polisi Tanzania FC, umeweka wazi kuwa, kuondoka kwa mshambuliaji, Ditram Nchimbi, hakutaathiri kiwango chao kwa sababu bado wana kikosi imara chenye uwezo wa kupambana na ushindani ulioko kwenye Ligi Kuu Bara.

Nchimbi ambaye alikuwa mmoja wa washambuliaji tegemeo katika kikosi cha Polisi Tanzania, amejiunga na Yanga katika kipindi cha dirisha dogo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa timu hiyo, Frank Lukwalo, alisema kuwa timu hiyo ina kikosi "kipana" na wanaamini wataendelea kuonyesha ushindani katika mechi mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Bado tuna kikosi kizuri, tunakiamini kwa asilimia 100, nafasi ya Nchimbi haina tatizo, tuna wachezaji wazuri ambao wana uwezo kama Ditram au zaidi, hivyo hatuna shaka," alisema Lukwalo.

Kiongozi huyo alisema kuwa tayari wameshasajili nyota wapya watatu katika dirisha dogo la usajili ambalo linaendelea, huku nyota wengine wakiwapandisha kutoka kwenye timu yao ya vijana.

"Wachezaji wengine ambao tuna mpango wa kuwasajili tutawachukua kutoka kwenye timu yetu ya vijana lengo ni kuifikisha mbali timu yetu," alisema Mtendaji huyo.

Aliwataka mashabiki wao waendelee kuwapa ushirikiano ili wafanye vema katika michezo mingine ya Ligi Kuu na mashindano ya Kombe la FA.

## Michuano kikapu Taifa kuanza leo

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya kuwania ubingwa wa Taifa wa mchezo wa kikapu maarufu "Mtaka Taifa Cup 2019" mwaka huu, yanatarajiwa kuanza leo mkoani Simiyu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Shirikisho la Kikapu Tanzania (TBF), Phares Magesa, alisema kuwa mashindano hayo yatakayomalizika Desemba 31, mwaka huu, yanatarajiwa kushirikisha timu kutoka mikoa yote ya Bara na Zanzibar.

Magesa alisema kuwa mashindano hayo yatashirikisha timu za wanawake na wanaume na pia kutakuwa na semina kwa viongozi wote wa vyama vya mikoa kuhusu masuala mbalimbali ya uongozi, utawala na masoko.

Magesa alisema kuwa lengo la kuandaa semina hiyo ni kuwaongezea viongozi wa mikoa uwezo wa kufanya shughuli zao za kila siku ambazo zinalenga maendeleo ya mchezo huo.

"Pia tunatarajia kuwa na mkutano mkuu utakaofanyika Desemba 29, mwaka huu. Pamoja na mambo mengine, mkutano huo utajadili na kupitisha mpango kazi wa TBF na kufanya mabadiliko ya katiba ya TBF," alisema Magesa.

Michezo
Ijumaa Desemba 27, 2019
Nipashe



Coutinho afikiria kurejea England HABARI UK.30



Mshambuliaji mpya wa Yanga, Yikpe Gnamien (kushoto), akiwa katika mazoezi ya timu hiyo baada ya kukamilisha mchakato wa usajili. Yanga inatarajia kuvaana na Tanzania Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa CCM Samora, Iringa. **PICHA: MTANDAO**

# KANYAGA KANYAGA YA MONDI YAGEUZA SOKOINE SHAMBA

## ●●● Rayvanny akoleza moto, Prisons vs Yanga sasa kupigwa Samora mjini Iringa...

**Na Isaac Kijoti,** MBEYA

BURUDANI kali iliyoshushwa katika Tamasha la Krismasi na Kundi la WCB, usiku wa kuamkia jana imeugeuza Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini hapa kuwa mithili ya shamba la mpunga kama si zizi la ng'ombe.

**Hali hiyo imesababisha mechi ya Ligi Kuu Bara, kati ya wenyeji Tanzania Prisons dhidi ya Yanga iliyokuwa ipigwe uwanjani hapo leo, Bodi ya Ligi kuihamishia Uwanja wa CCM Samora mjini Iringa.**

Akizungumza baada ya kupokea taarifa za mechi hiyo kuhamishiwa Uwanja wa Sokoine, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema wamelazimika kufunga safari jana mchana ili kuwahi kufika mkoani humo.

Hata hivyo, licha ya awali kabla ya taarifa hiyo, Bumbuli kueleza kuwa wataiandikia Bodi ya Ligi kudai fidia ya gharama zao za maandalizi ya mechi hiyo, alisema waмeelezwa bodi hiyo haitahusika na gharama zozote.

Kutokana na mabadiliko hayo ya uwanja, wadau wa soka wamemtupia lawama kubwa Meneja wa Uwanja wa Sokoine, Modestus Mwaluka, kwa kuruhusu tamasha hilo kufanyika uwanjani hapo wakati akijua kuna mchezo unaotakiwa kuchezwa siku moja baadaye. Kwa upande wake Meneja wa Uwanja, Mwaluka alisema alitoa taadhari muda mrefu kuhusu uharibifu wa uwanja utakaoweza kutokea kwa tamasha hilo kufanyika uwanjani hapo.

"Niliwaeleza wamiliki wa uwanja (CCM), lakini wakasema wataweka ulinzi wa kutosha kutoka Suma JKT kuwazuia watu wasiingie eneo la kuchezea, hivyo lawama hazipaswi kuelekezwa kwangu.

"Mimi ni msimamizi tu wa uwanja, wamiliki ni CCM, tutakachofanya ni kuhakikisha tunaukarabati mapema," alisema. "Uongozi wa uwanja unapaswa kuwajibika, kwanza tamasha hili lilikuwa la bure, kuna maeneo mengi ya wazi kwa nini wakubali lifanyike hapa?" Alihoji shabiki wa soka, Samsoni Mwakyusa.

John Manase, shabiki mpenzi mwingine wa soka, alisema: "Kwa hali hii sasa watatukosesha burudani za mechi maana uwanja huu lazima ufungiwe."

Katika tamasha hilo juzi, licha ya awali walinzi wa Suma JKT kujitahidi kuzuia umati wa wapenzi wa muziki waliohudhuria uwanjani hapo, mwanamuziki, Raymond Mwakyusa maarufu Rayvanny ndiye aliyekoleza moto zaidi kwa mashabiki kuingia uwanjani.

Baada ya Rayvanny kupanda jukwaani alisema "Kwa nini watu wanabanana na kule kuna nafasi? Acheni watu wafurahi."

Kauli hiyo ilisababisha maelfu ya mashabiki waliokuwa wamezunguka uwanja na wale waliokuwa jukwaani kumiminika eneo la kuchezea mpira na kuanza kucheza muziki, hivyo nyasi kugeuzwa tope.

Na ulipoimbwa wimbo wa "Kanyaga Kanyaga" na ule wa "Timua vumbi timua" hapo ndiyo uwanja ulipokanyagwa na kutimuliwa, hivyo kugeuzwa shamba la mpunga.

Katika tamasha hilo, ambalo pia lilihudhuriwa na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Diamond Platimum kutumbuiza jijini hapa, jambo ambalo lilisababisha maelfu ya wapenzi wa muziki kuhudhuria.

# Simba yapanga hesabu Ligi Kuu

**Na Somoe Ng'itu**

ZIKIWA zimebakia siku chake kabla ya watani wa jadi kukutana kwa mara ya kwanza katika msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amesema kuwa bado kikosi chake hakijaanza kuufikiria mchezo huo unaotarajiwa kuchezwa ifikapo Januari 4, mwakani.

Simba, inatarajia kushuka dimbani kesho kuwavaa KMC FC na Desemba 31, mwaka huu, itafunga mwaka kwa kuwakaribisha Ndanda FC, kutoka mkoani Mtwara.

Akizungumza na gazeti hili, Matola, alisema kuwa nguvu na akili zao kwa sasa ziko katika kuhakikisha wanashinda mechi mbili zilizo mbele yao na baada ya hapo, ndio wataanza mipango ya kuwakabili Yanga.

Matola alisema kuwa mechi zote za Ligi Kuu ni muhimu na ili timu iweze kutwaa ubingwa, inatakiwa kukusanya pointi nyingi.

"Kwanza kabisa tunamshukuru Mungu kwa kumaliza mechi salama, haikuwa mechi nyepesi, tumelazimika kubadilisha mbinu ili kupata ushindi, kuhusu Yanga, siwezi kuizungumzia kwa leo (juzi), tuna mechi nyingine hapo katikati, lakini kila mechi huwa na mipango yake," alisema Matola.

Nahodha huyo wa zamani wa timu hiyo aliongeza kuwa kila siku kikosi hicho kinaendelea kuimarika na wanaamini malengo yaliyowekwa na vinara hao wa Ligi Kuu Bara yatatimia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 04
9 770856 541002 >